# UMAASUMU WA MANABII

**Amani Iwe Juu yao**

## WOKOVU WAPATIKANAJE
## NA
## NINI HEKIMA YAKE HALISI

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

**Umaasumu wa Manabii[as]**

Tafsiri ya Kiswahili ya: 'Ismate Ambiyaa (Kiurdu)

'Ismate Ambiyaa (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza kwa Sura ya Makala (Kiurdu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2024

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-221-6
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# عصمتِ انبیاء علیہم السلام

---

# نجات کس طرح مل سکتی ہے
# اور اُس کی حقیقی فلاسفی کیا ہے

تصنیف

حضرت مرزا غلام احمد قادیانی

مسیح موعود و مہدی معہود علیہ السلام

# UMAASUMU WA MANABII

**Amani iwe juu yao**

## WOKOVU WAPATIKANAJE NA NINI HEKIMA YAKE HALISI

Mwandishi

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

# NENO LA MWENEZI

Mkononi mwenu mna 'Umaasumu wa Manabii[as], kilicho tafsiri ya makala ya Seyidna Ahmad[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, yaliyochapishwa ndani ya jarida 'Review of Religions (Kiurdu), toleo la Mei 1902.

Maana halisi ya umaasumu ni kutokuwa na dhambi. Maasumu ni mtu asiye na dhambi yoyote iwayo. Manabii wote ndio maasumu wanaojaliwa na Mwenyezi Mungu tabia ya kuchukia dhambi.

Yadaiwa kwamba Yesu pekee alikuwa maasumu, hivyo yeye tu aweza kuwa mwokozi. Lakini kila mwenye lubu anatambua kwamba umaasumu ni sifa nzuri hasi. Mwombezi hana budi kuwa na sifa chanya pamwe na sifa bora hasi. Na Mtume Muhammad[saw] aliwapita wanadamu wote katika sifa za aina hizi zote mbili, basi yu mwokozi hasa wa wanadamu wote. Ingawaje Manabii wote walikuwa na sifa hizo mbili sawa na hali zao, nao walikuwa waokozi katika zama zao, lakini Mtume[saw] alikuwa na sifa hizo kwa wingi na kwa ubora zaidi kuliko wengine – historia ya maisha yake yahakikisha jambo hili kwa uwazi mno – na tena sheria yake ni kwa ajili ya

wanadamu wote na itadumu hadi siku ya Kiyama, hivyo yeye ndiye mwokozi wa wanadamu wote.

Kitabuni humu mmeelezwa haja ya uombezi, pia tofauti baina ya dhambi na uhalifu na kadha wa kadha. Upinzani fulani wa Wakristo pia umejibiwa namna inavyowanyamazisha kabisa.

Kitabu hiki – kama vilivyo vitabu vyote wa Seyidna Ahmad[as] – kimejaa elimu tele ya ndani ya hali ya juu, ifaayo kuzingatiwa.

Kitabu hiki kimefasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, nami nimeidurusu tafsiri hii kuisogeza karibu zaidi na matini ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain alipanga herufi hizi kwa kompyuta na kutayarisha fomati. Mungu Awabariki wote waliohusika na kazi hii bora.

Namwomba Mola Mtukufu Akifanye kitabu hiki kiwe chenye kuwanufaisha wasomaji kielimu na kiroho. Amin.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 25 Januari 2023

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

# Wokovu Wawezaje Kupatikana na ni Nini Hekima yake Halisi?

Kati ya masiala ya dini, masiala ya wokovu na uombezi ni masiala adhimu na mazito kiasi hiki kwamba makusudio yote ya kufuata dini yanaishia kwake. Na kwa kupima uhalisi na ukweli wa dini yoyote, masiala hayo ndiyo ishara safi na wazi ambayo kwayo kwa utulivu kamili yaweza kujulikana kwamba dini fulani kwa hakika ni kweli na imetoka kwa Mungu. Na ni kweli kabisa na sahihi kwamba dini isiyoyaeleza masiala haya sawasawa au haikuweza kuonyesha waziwazi kwa upambanuzi dhahiri mifano iliyopo hivi sasa ya waliookoka wa dhehebu lake, kwa ubatili wa dini hiyo hakuna haja ya dalili nyingine. Lakini dini iliyobainisha uhakika halisi barabara wa wokovu, na sio kiasi hiki tu, bali imetuonyesha pia katika zama zake hizi watu waliopuliziwa kikamilifu roho ya wokovu, dini hiyo imepiga muhuri juu ya ukweli wake na kwamba imetoka kwa Mungu.

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

Ni dhahiri kwamba kila mtu kitabia huhisi moyoni mwake kwamba kwa sababu ya namna mbalimbali za mighafala, mapazia, mashambulizi ya nafsi, makosa, udhaifu, ujahili, giza kwenye kila hatua, kujikwaa, hatari za kufululiza na wasiwasi, na pia kwa maafa ya aina aina ya dunia na mabalaa analazimika kuhitaji Mkono wenye nguvu ambao umwokoe katika mambo hayo yote makuruhu. Kwani, mwanadamu yu dhaifu kitabia, naye hawezi kuitegemea nafsi yake hata kwa kitambo kidogo kwamba aweza kutoka mwenyewe katika giza la kinafsi. Huu ni ushahidi wa dhamiri ya mtu. Isitoshe, tukitafakari, maarifa ya kawaida pia hutaka kwamba mwombezi huhitajika kwa wokovu, kwani Mwenyezi Mungu Yupo kwenye daraja ya juu kabisa ya utukufu na utakaso na mwanadamu yumo shimoni mwa giza kabisa, uasi na uchafu. Na kwa kukosa mnasaba na mshabaha, watu wa kawaida hawawezi kujipatia daraja ya wokovu kwa kujaliwa moja kwa moja ukarimu wa Mwenyezi Mungu. Basi, hekima na rehema ya Mungu ilitaka kwamba miongoni mwa binadamu baadhi ya watu wakamilifu wawe njia ya kati ambao wanao ubora mahususi katika asili yao. Na hao wawe watu ambao asili yao imejichukulia sehemu fulani ya sifa za kiungu na sehemu fulani ya sifa za kibinadamu ili kwa mnasaba wa kiungu wajipatie baraka kutoka kwa Mungu, na kwa mnasaba wa kibinadamu wazifikishe upande wa chini, yaani kwa

wanadamu, zile baraka walizozipata kutoka juu. Na ni sawa kabisa kusema kwamba wanadamu kama hao kwa sababu ya kuzidi katika ukamilifu wa sifa za kiungu na za kibinadamu wanapambanuka baina ya wanadamu wengine, kana kwamba hao ni viumbe tofauti. Kwani, kiasi wanachojaliwa jazba kwa kudhihirisha ujalali na adhama ya Mungu na kiasi wanachojazwa uaminifu mioyoni mwao, na kisha kiasi wanachopewa jazba ya kuwahurumia wanadamu, ndilo jambo la kuzidi kawaida ambalo ni vigumu kwa wengine hata kufikiria juu yake. Naam, yafaa pia kukumbuka kwamba watu hao wote hawawi katika daraja moja, bali katika ubora wa asili mtu fulani yupo kwenye daraja ya juu kabisa na mwingine kwenye daraja ndogo kuliko yake, na mwingine, ndogo kuliko yake. Dhamiri safi ya mwenye akili ya kawaida yaweza kuelewa kwamba masiala ya uombezi siyo masiala ya bandia na ya kubuniwa, bali tangu mwanzo mpango uliowekwa na Mungu ipo mifano yake, na ndani ya kanuni ya ulimwengu wapatikana ushahidi wake waziwazi.

Sasa, yafaa kuelewa hekima ya uombezi kwamba شَفْع katika lugha yamaanisha 'jozi'. Basi, neno شَفَاعَت (uombezi) laashiria kwenye hii ya kuwa jambo linalolazimika kuwemo katika sifa za mwombezi ni kwamba yeye awe anaungana na pande mbili. Yaani, kwa upande mmoja awe na uhusiano imara kabisa na

Mwenyezi Mungu, kana kwamba kwa sababu ya mwungano kamili awe kwa Mungu kama kiungo, na kwa upande wa pili aungane kabisa na mahuluku, kana kwamba yu sehemu ya viungo vyao. Basi, kwa uombezi kuathiri, kwa hakika, hizi ndizo sehemu mbili zilizo msingi wa athari kupatikana. Hii ndiyo siri kwamba Mungu Alimwumba Adamu hivi kwamba tangu mwanzo wa uumbaji Akaweka uhusiano wa aina mbili katika tabia yake; yaani uhusiano mmoja Akaimarisha kwa Mungu jinsi Alivyosema katika Kurani Tukufu فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا لَهُ سَٰجِدِينَ[3], yaani Nitakapomkamilisha na kumpulizia roho Yangu, papo hapo, Enyi Malaika, mmwangukie kumtii.[4] Kutokana na aya hii, iliyotajwa juu, inathibitika

[3] Sura Al-Hijr 15:30

[4] Katika aya hii, imeashiriwa kwenye siri ya ndani iliyo ishara ya ukamilifu wa hali ya juu, nayo ni hii kwamba mwanzoni mwanadamu huwa sura tu ya binadamu, lakini ndani mwake hamna uhai wala hamna ruhania. Katika hali hii Malaika hawamtumikii, kwani yu ganda tu pasipo kiini. Lakini baadaye pole pole mtu mwema hufikiwa na zama anapomsogelea sana Mungu, hapo nafsi yake inapopata kutazamana barabara na mwanga wa Mungu Jalali, na haibaki katikati pazia yoyote izuiayo mwanga ule, hapo mara moja mwanga wa Uungu tunaoweza kuuita, kwa maneno mengine, roho ya Mungu, humwingia mtu huyo. Na hii ndiyo hali mahususi ambayo kuihusu hiyo imesemwa katika Neno la Mungu kwamba Mungu Alimpulizia Adamu roho yake. Katika hali hii bila kujikalifisha wala kwa jambo linalokuwa kama namna

waziwazi kwamba Mungu Akimpulizia Adamu roho Yake wakati wa kumwumba, Akaiwekea asili yake uhusiano Naye. Hii ilifanywa ili mwanadamu kiasili apate

---

ya amri za sheria, Malaika wanaamrishwa kumwangukia katika sijida, yaani kumtii kikamilifu kana kwamba wanamsujudia. Amri hii huwa inaambatana na asili ya Malaika, si jambo geni. Yaani, kwa mtu ambaye dhati yake inakuwa juu ya sura ya Mungu, Malaika wenyewe kitabia wanahisi kwamba tumwangukie sasa kumtumikia. Na visa kama hivyo kwa kweli sio visa tu, bali katika Kurani Tukufu imo suna hii ya Mungu kwamba ndani ya visa hivyo unakuwemo uhakika fulani wa kielimu. Basi, katika sehemu hii upo uhakika huu wa kielimu kwamba Mwenyezi Mungu Ametaka kudhihirisha kwa njia ya kisa hiki kwamba kuna alama gani ya mtu mkamilifu. Basi, Akasema kwamba alama ya mtu mkamilifu ni kwamba yeye asiwe mwenye bahati ndogo katika sehemu yoyote ya umbo la kibinadamu, na viungo vyake vya kiroho na kimwili viwe vimepata sehemu kamili katika umbo la kibinadamu na tabia yake iwe katika hali ya wasitani kabisa. (2) Na alama ya pili ni kwamba roho ya Mungu iwe imeingia ndani mwake. (3) Na alama ya tatu ni kwamba Malaika wamsujudie, yaani Malaika wote wanaoshughulikia mambo ya ardhi na mbingu, wamhudumie na wafanye kazi atakavyo. Jambo halisi ni hili kwamba Mwenyezi Mungu Anapokuwa pamoja na mja fulani, basi jeshi lake lote la Malaika pia linakuwa pamoja na mja huyo na linamwinamia. Basi, katika kila uwanja na wakati wa kila shida Malaika humsaida na wanajiweka tayari kila saa kumtii kana kwamba saa zote humsujudia, kwani yu Khalifa wa Mungu. Lakini watu wa mawazo ya kidunia hawawezi kuyaelewa mambo haya, kwani hawakujaliwa sehemu katika roho ya kimbingu. Mwandishi.

kuhusiana na Mungu. Kadhalika, kwa upande wa pili, ililazimika pia kwamba uhusiano wa kiasili ufanyike pia kwa watakaoitwa wanadamu, kwani umbo lao litakapokuwa ni mfupa kutoka katika mfupa wa Adamu, na nyama kutoka katika nyama yake, basi lazima watapata sehemu katika roho yake pia aliyopuliziwa Adamu. Hivyo, kitabia Adamu atakuwa mwombezi wao. Kwani, unyofu iliojaliwa tabia ya Adamu kwa kupuliziwa roho, ni lazima sehemu fulani ya unyofu wake apate mtu yule pia aliyetoka kutoka ndani mwake, kama vile ilivyo dhahiri kwamba mtoto wa kila mnyama anachukua sehemu katika sifa na matendo yake. Na kwa kweli, uhakika wa uombezi pia ni huu huu kwamba mrithi wa kiasili apate sehemu katika mrithiwa wake. Kwani, hivi punde tumeshaeleza kwamba neno شَفَاعَت (uombezi) limetokana na neno شَفْع linalomaanisha 'jozi'. Basi, mtu atakayekuwa kiasili jozi ya mtu mwingine lazima atapata sehemu katika sifa zake. Kwa msingi huu nidhamu yote ya kurithi sifa inaendelea, yaani mtoto wa mwanadamu hupata sehemu katika sifa za kibinadamu na mwanafarasi hupata sehemu katika sifa za farasi na mwanambuzi hupata sehemu katika sifa za mbuzi; na urithi huu kwa maneno mengine huitwa kufaidika na شَفَاعَت (uombezi), kwani شَفَاعَت latokana na شَفْع (shaf') yaani زَوْج (jozi). Basi msingi wote wa kufaidka na شَفَاعَت (uombezi) hulitegemea jambo hili

kwamba anayetaka kufaidika na uombezi wa mtu, basi awe na uhusiano naye wa kiasili ili iliyojaliwa asili yake, ipatikane pia kwa asili ya huyo. Uhusiano huu kama vile ulivyokuwemo katika asili ya kibinadamu kama kipaji – kwani mtu mmoja ni sehemu ya mtu mwingine – ndivyo hivyo unavyoongezeka uhusiano huu kwa juhudi pia. Yaani, mtu anapotaka kwamba huba na huruma ya kiasili kwa wanadamu iliyomo ndani mwake iongezeke, basi yaongezeka pia kadiri ya wasaa wake wa kitabia na sawa na mnasaba wake. Hii hii ndiyo sababu ya mfuro wa mawimbi ya nguvu ya mapenzi kwamba mtu anazidisha huba ya mtu mwingine kiasi hiki kwamba hawezi kupata utuvu bila kumwona. Hatimaye, mapenzi yake makali yanaathiri moyoni mwa mtu huyo mwingine pia. Na anayempenda sana mno mwingine, huyu hutaka kikamilifu na kwa ukweli wema wake. Jambo hili lashuhudiwa na kujulikana kutoka kwa mama wazazi kuhusu watoto wao. Basi, mzizi wenyewe wa uombezi ni huba hii hii inapokuwa na uhusiano wa kiasili pia pamoja nayo, kwani pasipo uhusiano huo wa kiasili, ukamilifu wa huba, ulio sharti la uombezi, hauyumkiniki. Kwa kuingiza uhusiano huu ndani ya asili ya kibinadamu, Mungu Hakumwumba Hawa moja kwa moja, bali akamtoa

kutoka katika ubavu wa Adamu, kama Alivyosema katika Kurani Tukufu خَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا[5] , yaani kutoka katika mwili wa Adamu tukamwumba mwenzake aliye Hawa, ili uhusiano huu wa Adamu kwa Hawa na kizazi chake uwe wa kiasili, si wa kubuniwa. Na alifanya hivyo ili kuhusiana kwa wanadamu wao kwa wao na kuhurumiana kwao kudumu. Kwani, uhusiano wa kiasili huwa hautanguki, lakini uhusiano usio wa kiasili haudumu, kwani hauna mvuto ule unaokuwa katika uhusiano wa kiasili. Ilmuradi, Mungu Aliumba uhusiano wa aina mbili wa Adamu uliopaswa kuwepo kwa Mungu na kwa wanadamu. Basi, kwa maneno haya ni wazi kabisa kwamba mtu mkamilifu afaaye kuwa mwombezi aweza kuwa yule tu aliyepata sehemu kamili ya uhusiano huu wa aina mbili, na mtu yeyote bila ukamilifu wa aina hizo mbili; hawezi kuwa mtu mkamilifu. Kwa hiyo, baada ya Adamu, suna hii ya Mungu inaendelea hivi kwamba kwa mtu mkamilifu anayeweza kuwa mwombezi, uhusiano huu wa aina mbili ukalazimishwa kuwepo, yaani uhusiano mmoja huu kwamba roho ya kimbingu ilipulizwa ndani mwao, na Mungu Akaungana nao hivi kana kwamba Akashuka ndani mwao. Na wa pili ndio huu kwamba muungano wa usuhuba wa binadamu ulioimarishwa kati ya Hawa na

---

[5] Sura An-Nisaa 4:2

Adamu kwa huba na huruma ukanga'rishwa zaidi kuliko wote. Kwa sababu hii hii wakapata mwelekeo kwa wake zao, na hii ndiyo alama ya kwanza ya jambo hili kwamba wanayo jazba ya kuwahurumia wanadamu; na kwenye hii hii Hadithi ile inaashiria ambayo maneno yake ni haya: خَيْرُكُمْ خَيْرُكُمْ بِأَهْلِهِ , yaani kati yenu yule tu anaweza kuwa mwenye kuwatendea binadamu mema zaidi kuliko wote ambaye kwanza awe anamtendea mkewe mema. Lakini amtendeaye mkewe dhuluma na shari haiyumkini aweze kuwatendea wengine pia mema. Kwani, Mungu Akimuumba Adamu, kwanza kabisa Akamfanya mkewe apate kupendwa naye. Basi, mtu asiyempenda mkewe, au hana mke kabisa, ameanguka kutoka kwenye daraja ya mtu mkamilifu na limekosekana sharti moja kati ya masharti mawili ya uombezi. Hivyo, hata kama yeye hana dhambi, hata hivyo hafai kufanya uombezi. Lakini, anayeoa mke, hujiwekea msingi wa huruma ya binadamu, kwani mke anasababisha jamaa wengi; watoto wanazaliwa, nao wanawaoa wake zao, na watoto wanakuwa na nyanya na wajomba na kadhalika. Na hivyo mtu kama huyo huzoea tu kupenda na kuhurumia, na daraja ya mazoea yake ikipanuka huwatolea wote hadhi ya huruma yake. Lakini watu wanaokulia kama *majogi* – wanaojitenga na mambo ya dunia, wala hawaoi –

hawapati nafasi ya kupanua mazoea yao, kwa hiyo nyoyo zao hubaki kuwa ngumu na kavu.

Na umaasumu hauhusikani hasa na uombezi, kwani maana ya umaasumu ni kiasi hiki tu kwamba mtu aepukane na dhambi; na ufafanuzi wa dhambi ni huu kwamba mtu akivunja kwa kusudi amri ya Mungu astahili kuadhibiwa.[6] Basi ni dhahiri shahiri kwamba umaasumu

---

[6] Kwa kuwa sawa na akili na uadilifu, ufafanuzi wa dhambi ni huu kwamba kitendo fulani kitaitwa ni dhambi ambapo mtu kwa kitendo kile akivunja amri ya Mungu astahili kuadhibiwa. Hapo katika hali hii imelazimika kwamba kabla ya kutendeka dhambi, amri ya Mungu iwepo na pia amri ile iwe imemfikia tayari mtenda dhambi, na vile vile kumhusu mtenda kitendo kile akili iweze kupendekeza kwamba kwa kutenda kitendo hiki kwa hakika yeye ameshastahili kuadhibiwa. (Mifano ya wasiohesabiwa kuhalifu): Zaid yupo katika nchi ya mbali ambapo sheria ya Mungu haijamfikia. Kama katika amri za sheria ameivunja amri moja au amri chache, basi kwa uvunjaji huu wa amri za Mungu yeye si mhalifu, kwani hajapata habari ya sheria hii. Lakini kama Zaid kwa hali ya kuwa na akili na ufahamu aanze kuabudu masanamu na aachane na tauhidi, basi juu ya kuwa sheria haijamfikia, hata hivyo yu mhalifu, kwani tauhidi iliyoletwa na Kurani siyo kama Utatu wa Wakristo usiokuwa umenakishiwa katika tabia ya asili ya binadmau, bali tangu azali imenakishiwa katika asili ya binadamu. Kwa hiyo, kwa kuivunja hailazimu sheria iwe imemfikia; yalazimu tu akili ya mtu iwepo. Lakini, kama sheria ipo na imemfikia mtu, lakini yeye hajabalehe au yu majununi, na katika hali hii akatenda kitendo


na uombezi havilazimiki kutangamana, kwani sawa na ufafanuzi uliotajwa hapo juu, watoto wasiobalehe, na majununi wa kuzaliwa pia, hawana dhambi, sababu yake ni kwamba hawana uwezo wa kutenda dhambi kwa kusudi, wala mbele ya Mwenyezi Mungu hawastahili kuadhibiwa kwa kutenda kitendo fulani. Basi, bila shaka wanayo haki waitwe maasumu. Lakini, je wanayo haki hii pia kwamba waitwe kuwa waombezi wa watu na wakombozi? Basi, ni dhahiri kwayo kwamba hamna uhusiano wowote wa kweli baina ya mkombozi na maasumu, na kamwe akili haiwezi kufahamu kwamba kutokuwa na dhambi kuna uhusiano wowote wa kweli na uombezi. Naam, akili yafahamu vizuri kwamba kwa mwombezi ni lazima kwamba uhusiano wa aina zote mbili zilizotajwa juu ziwepo ndani yake. Na akili bila kusita yahukumu kwamba ikiwa mtu anazo sifa hizi mbili kwamba kwanza awe na uhusiano imara na Mungu, na upande wa pili, kwa kiumbe pia uhusiano uwe wa huba na huruma, basi bila shaka mtu kama huyo atawafanyia, kwa jazba ya moyo, uombezi watu ambao hawakuvunja uhusiano Naye kwa kusudi, na uombezi wake ule utakubaliwa. Kwani, mtu ambaye asili yake imejaliwa

---

kinachoitwa dhambi sawa na sheria, hapo hapaswi kuadhibiwa kwani hakupewa akili, kwa hiyo juu ya kuwapo sheria, yeye hana dhambi. Mwandishi

uhusiano wa aina hizo mbili, natija yake ya lazima ni kwamba kwa sababu ya huba timilifu ya Mungu avute baraka ile, na kisha kwa huba kamilifu ya mahuluku awafikishie baraka ile, na hali iyo hiyo kwa maneno mengine huitwa uombezi. Kwa mwombezi, nilivyoeleza sasa hivi, ni lazima kwamba awe na uhusiano imara na Mungu kana kwamba Mungu Ameshamshukia moyoni mwake; na kwa kufa kwa ubinadamu wake wote, mng'ao wa kiungu upate kuzalika katika kila unywele wake; na roho yake ikiyeyuka kama maji, itiririke kwa upande wa Mungu na hivyo iwe imefikia kilele cha ukaribu wa Mungu. Na kwa mwombezi yalazimu pia kuwa moyo wake uwe umenaswa katika huruma ya yule ambaye mwombezi anataka kumwombea kana kwamba karibuni atazimia, na kana kwamba kwa mahangaiko makubwa viungo vyake vinatengana naye na hisia zake zimesambaratika, na huruma yake ikamfikishia daraja ile iliyozidi kuliko baba na kuliko mama na kuliko kila mfariji. Hali hizi mbili zitakapozalika ndani yake na atakuwa hivi kana kwamba kwa upande mmoja ameungana na eneo la tabia ya kiungu na kwa upande wa pili ameungana na eneo la tabia ya kibinadamu, ndipo pande zote mbili za mizani zitakuwa sawa ndani yake. Yaani, yeye atakuwa dhihirisho la tabia ya kiungu

kikamilifu na dhihirisho la tabia ya kibinadamu kikamilifu pia, na atakuwa kama mwungano baina ya hali mbili, hivi:




Kwenye daraja hii hii ya uombezi Mungu Ameashiria katika Kurani Tukufu na kusema kuhusu shani ya Mtume[saw] kuwa mwombezi: دَنَا فَتَدَلّٰى فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ اَوْ اَدْنٰى[7]. Yaani, Mtume huyu akapaa kuelekea kwa Mungu na kumkaribia Mungu hadi iwezekanayo na kapita daraja zote za ukamilifu wa ukaribu wa Mungu na akapata hadhi kamili katika eneo la kiungu; kisha akarejea kikamilifu kwa eneo la kibinadmau, yaani akajifikisha mpaka sehemu ya mwisho ya utumishi na akapata hadhi kamili katika sifa

[7] Sura An-Najm 53:9-10

tukufu za lazima za kibinadamu, yaani katika huruma na huba ya binadamu ziitwazo ukamilifu wa tabia ya binadamu. Hivyo, kwa upande mmoja akafikia ukamilifu katika huba ya Mungu na kwa upande wa pili katika huba ya binadumu. Basi kwa vile akamkaribia Mungu kwa ukamilifu kisha akawakaribia binadamu kikamilifu, hivyo kwa sababu ya ukaribu wake ulio sawa baina ya pande zote mbili akawa kama mstari wa katikati baina ya pinde mbili. Hivyo, basi, sharti lile lililolazimu kwa uombezi limepatikana ndani yake, na Mungu Amemshuhudia katika Neno Lake kwamba yupo katikati ya wanadamu na Mungu wake kama ulivyo utari baina ya pinde mbili.

Na tena katika sehemu nyingine akasema kuhusu kumkaribia Mungu hivi: قُلْ اِنَّ صَلَاتِيْ وَ نُسُكِيْ وَ مَحْيَايَ وَ مَمَاتِيْ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ[8], yaani wapashe watu habari kwamba hali yangu ni hii kwamba nimepotewa kabisa na dhati yangu, ibada zangu zote zimekuwa kwa ajili ya Mungu. Hii yaashiria kwenye jambo hili kwamba kila mtu maadamu hajakamilika, hawezi kufanya ibada halisi ya Mungu; bali ibada yake kidogo huwa kwa Mungu na kidogo kwa nafsi yake, kwani anatamani adhama na utukufu wa nafsi yake jinsi ipasavyo kumwadhimisha Mungu na kumtukuza. Na huu huu ndio uhakika wa ibada. Na kadhalika sehemu moja ya ibada yake inakuwa kwa mahuluki, kwani adhama,

[8] Sura Al-An'aam 6:163

utukufu, nguvu na madaraka vinavyopaswa kuwekwa mahususi kwa Mungu, anawapa mahuluku sehemu ya adhama hiyo na uwezo wake. Kwa hiyo, jinsi anavyomwabudu Mungu, hujiabudu nafsi yake na pia huwaabudu mahuluku, bali kwa jumla anazipa nyenzo zote duni sehemu katika ibada yake, kwani anafikiria kwamba hizo nazo zaingilia kati mpango wa kuharibu na kuimarisha. Basi, mtu hawezi kuwa mwabudu Mwenyezi Mungu kwa kweli ambaye mara anajifanya nafsi yake mshirika katika adhama ya Mungu, na mara anawafanya mahuluku washirika na mara nyenzo; bali mwabudu wa kweli ni yule anayempa Mungu pekee adhama zote za Mungu na utukufu wote na mamlaka yote, si mwingine yeyote awaye. Na ibada ya mtu ifikiapo daraja hii ya tauhidi, hapo ndipo kwa hakika yeye anaweza kuitwa mwabudu Mungu. Na mtu kama huyo jinsi anavyosema kwa ulimi kwamba Mungu ndiye Mmoja ambaye hana mshirika, ndivyo hivyo kwa kitendo chake, yaani kwa ibada yake, pia anavyoshuhudia tauhidi ya Mungu. Basi kwenye daraja hiyo kamili imeashiriwa katika aya iliyotajwa juu kumwambia Mtume Mtukufu[saw] kwamba waambie watu kuwa ibada zangu zote ni kwa Mungu, yaani nafsi, mahuluku na nyenzo havina sehemu katika ibada yangu.

Kisha baada yake akasema kwamba dhabihu yangu pia ni kwa Mungu pekee, na uzima wangu pia ni kwa Mungu, na kufa kwangu pia ni kwa Mungu. Kumbukeni kwamba نَسِيْكَة (*nasikah*) katika lugha ya Kiarabu huitwa dhabihu, na neno نُسُك (*nusuk*) lililomo katika aya ni wingi wake, na maana yake ya pili ni ibada pia. Basi, hapa neno limetumika ambalo lina maana zote mbili za ibada na dhabihu. Hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba ibada kamili ambamo nafsi, mahuluku na nyenzo havishiriki, kwa kweli ni dhabihu; na dhabihu kamili kwa hakika ni ibada kamili. Kisha aliyosema baada yake kwamba uzima wangu pia ni kwa Mungu na kufa kwangu pia ni kwa Mungu, sentensi hii ya mwisho ni sherehe ya neno dhabihu ili mtu yeyote asidhani kwamba maana ya dhabihu ni dhabihu ya mbuzi, au dhabihu ya ng'ombe, au dhabihu ya ngamia, na ili kwa maneno haya 'uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mungu pekee' ifahamike bayana kwamba muradi wa dhabihu hii ni dhabihu ya roho. Na neno قُرْبَانِ – kurbani – (dhabihu) limetokana na neno قُرْب – kurb – na hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba ukaribu wa Mungu unapatikana ambapo nguvu zote za nafsi na matamanio ya nafsi zifikiwe na mauti. Ilmuradi, aya hii ni dalili kubwa juu ya ukaribu mtimilifu wa Mtume Mtukfu[saw]. Na aya hii inaeleza kwamba Mtume Mtukfu[saw] alijipoteza na kutoweka ndani mwa Mungu hata kwamba pumzi zote za

uhai wake na kifo chake kikawa kwa ajili ya Mungu tu, na ndani ya dhati yake haikubaki sehemu yoyote ya nafsi, mahuluku na nyenzo, na roho yake iliangukia kizingitini pa Mungu kwa ikhlasi kiasi hiki kwamba haikubaki ndani mwake mchanganyiko hata kidogo wa kitu kingine, hivyo akatimiliza sehemu moja ya sharti la lazima kwa mwombezi. Na sentensi ya mwisho ya aya iliyotajwa juu ni hii kwamba uzima wangu na kufa kwangu ni kwa Mungu aliye Mola wa ulimwengu wote, humo mna ishara hii kwamba dhabihu yangu pia ni kwa ajili ya heri ya ulimwengu wote. Kadhalika, sehemu ya pili ya sharti la uombezi ni kuwahurumia mahuluku, nasi sasa hivi tumeandika kwamba neno la pili, تَدَلّٰى , latokana na neno دَلْو – dalwun – na maana ya دَلْو ni kuzamisha ndoo katika kisima ili ijae maji; na maana ya pili ya دَلْو ni kumshika mtu fulani kuwa mwombezi. Basi تَدَلّٰى lamaanisha kuwaelekea watu walio mbali kwa huruma kamili na kuwafariji ili kuwafanyia uombezi, kwa kuyaondolea mbali maji yao machafu na kuwapatia maji safi.

Kwa vile kumpenda Mungu na kufikia daraja ya juu kabisa katika huba Yake ni jambo asiloweza mwingine yeyote kupata habari yake, kwa hiyo Mwenyezi Mungu Akadhihirisha zile amali za Mtume Mtukufu[saw] ambazo kwazo yathibitika kwamba Mtume Mtukufu[saw] kwa hakika alimtanguliza Mungu juu ya vitu vyote, na katika

kila chembe ya mwili wake na kiungo chake huba ya Mungu na adhama Yake ilikuwa imechanganyika kana kwamba dhati yake ilikuwa kama kioo kwa kushuhudia kikamilifu ming'ao ya Mungu. Alama za huba kamili ya Mungu, kadri akili inayoweza kuzifikiria, zote zilikuwepo ndani ya Mtume Mtukufu[saw]. Hii ni dhahiri kwamba mtu mmoja anayempenda mtu mwingine, anampenda kwa sababu ya hisani yake fulani au kwa uzuri wake. Kwani, tangu mwanadamu alipozaliwa mpaka leo, binadamu wote wameafikiana juu ya tajriba hii kwamba hisani huhamasisha huba. Na ingawaje wanadamu wanahitilafiana kitabia, hata hivyo ndani ya wanadamu wote sifa hii imo kwamba sawa na uwezo wao lazima kwa kuathirika na hisani hujipatia huba ya mhisani moyoni hata kwamba kundi la watu wabaya sana, wenye mioyo migumu na duni ambao ni wezi, majambazi na wahalifu wanaojichumia riziki kwa hatia mbalimbali, pia huathirika na hisani. Kwa mfano, mwizi atoboaye ukuta wa nyumba ili kuiba, akipata nafasi usiku kuiba nyumba mbili, na kati ya wenye nyumba hizo mbili mmoja awe aliyemfanyia mema wakati fulani, na wa pili ni mgeni kabisa, hapo asili ya mwizi juu ya kuwa mbaya sana haitapenda wakati wa kuiba kuacha kusudi nyumba ya mgeni na kutoboa ukuta wa nyumba ya rafiki yake; bali achilia mbali wanadamu, hata wanyama na pia wanyama wala nyama wanayo sifa hii kwamba hawamshambulii

mhisani. Kuhusu jambo hili watu wengi wameishuhudia tabia na sifa ya mbwa jinsi anavyomtii mhisani wake. Basi, hakuna shaka yoyote ndani yake kwamba hisani husababisha huba. Kadhalika uzuri kusababisha huba pia ni dhahiri, kwani katika kushuhudia uzuri kuna ladha na mwanadamu kiasili huelekea kwenye kitu kinachompa ladha. Na uzuri haumaanishi sura ya mwili pekee kwamba jicho liwe hivi, pua liwe hivi, na paji la uso liwe hivi, na rangi iwe hivi; bali muradi wake ni uzuri wa asili, na ukamilifu wa asili, na ulainifu wa asili uliopo katika hali ya wasitani na usio na kifani, usabibishao kuzalika mvuto ndani yake. Basi mazuri yoyote inayoyasifu tabia ya asili ya mtu ndio uzuri, na moyo wa mtu huvutika kwake. Mathalan, mtu fulani ni mpigaji mweleka, shujaa, mashuhuri ambaye mtu yeyote hawezi kuwa sawa naye katika mweleka, na siyo hiyo tu bali anaweza kuwakamata simba pia kwa mkono, na ndani ya medani ya vita anaweza kushinda watu elfu kwa ushujaa na nguvu yake, na akihusuriwa na maelfu ya maadui anaponyoka kwa kujiokoa, basi mtu kama huyo kitabia atavutia mioyo na lazima watu watampenda. Na ingawaje watu wasinufaike kitu na mweleka wake usio na kifani na ushujaa wake, bali awe mkazi wa nchi ya mbali ambaye hata hawajamwona, au awe amepita kabla ya zama hizi, hata hivyo watu watasikiliza visa vyake kwa huba na kumpenda kwa ukamilifu wake huu. Basi, ni nini sababu

ya huba hii? Je, amemfanyia yeyote hisani? Ni dhahiri, hajamfanyia yeyote hisani; basi, hakuna sababu yake nyingine isipokuwa uzuri wake. Hakuna shaka kwamba sifa hizi zote za kiroho zinahesabiwa katika uzuri na zaitwa hulka njema na sifa njema zinazokabiliana na uzuri wa viungo. Tofauti kati ya hulka njema na sifa njema ni hii kwamba hulka njema au sifa njema ya mtu itaitwa hisani kwa mtu ambapo mtu huyo ameishanufaika na hulka njema na sifa njema hiyo na kupata faida yake. Basi, mtu atakayejifaidisha na hulka njema hii na sifa njema, kulingana naye hulka njema na sifa njema hiyo itakuwa hisani ambayo ataitaja kumsifu na kumshukuru. Lakini kwa watu wengine hulka njema hiyo itakuwa ni uzuri wake. Kwa mfano, sifa ya ukarimu na upaji ni hisani kwa ajili ya mtu aliyefaidika nao, lakini machoni pa wengine hiyo itafahamika kuwa ni sifa njema.

Ilmuradi, kanuni ya Mungu na pia utaratibu wa ulimwengu unaoendelea tangu kale na tangu chanzo cha binadamu unatufundisha kwamba kwa kuzalika uhusiano imara na Mungu hakuna budi kupata kunufaika na hisani na uzuri Wake. Na sasa hivi tumeshaandika kwamba hisani yamaanisha mifano ya hulka za Mungu aliyoishuhudia mtu kujihusu kwa macho yake mwenyewe. Kwa mfano, wakati wa kutojiweza, unyonge, umaskini na uyatima, Mungu Akamsimamia; na wakati wa mahitaji

Mungu Mwenyewe Akamtimiliza haja zake; na wakati wa huzuni zisizovumilika Mungu Mwenyewe Akamsaidia, na wakati wa kumtafuta Mungu, Mungu Mwenyewe Akamwongoza pasipo kupitia kiongozi na mwongozi yeyote. Na muradi wa uzuri pia ni sifa nzuri zile zile za Mungu zinazoonekana kwa sura ya hisani pia. Mathalan, kudura kamili ya Mungu, upole, uraufu, ulezi na rehema; na ulezi wake kwa watu wote unaoshuhudiwa; na neema zake za kawaida zilizopo kwa wingi kwa starehe ya wanadamu; na elimu yake anayoipata mtu kupitia Manabii Wake na kusalimika na mauti na maangamio; na sifa Yake ya kukubali maombi ya wahangaikao na wasumbukao; na uzuri Wake huu kwamba watu wamwelekeao, Yeye Huwaelekea zaidi kuliko wao – sifa hizo zote za Mungu zaingia katika uzuri wake. Kisha ni sifa hizo hizo kwamba mtu anapofaidika pia hasa nazo, hapo hizo zaitwa hisani pia kwa ajili yake, ingawa kwa wengine hizo ni uzuri wake tu. Na mtu anayezishuhudia sifa hizo za Mwenyezi Mungu, zilizo kwa hakika uzuri wake, kwa sura ya hisani pia, hapo imani yake huimarika sana sana, naye huvutika kwa Mungu kama vile chuma huvutika kwa sumaku. Huba yake kwa Mungu yaongezeka sana na mategemeo yake juu ya Mungu yanaimarika mno. Na kama vile hupata tajriba ya kwamba heri yake yote imo katika Mungu, kwa hiyo matarajio yake kwa Mungu yaimarika sana, na kitabia, pasipo

kujikalifisha wala kujisingizia, yuadumu kuelekea kwa Mungu, na muda wote hujiona mhitaji wa msaada wa Mungu. Na ana yakini kwa kufikiria sifa Zake hizo kamili kwamba lazima atafaulu, kwani mifano mingi ya baraka, ukarimu na upaji wa Mungu ameishaishuhudia kwa macho yake. Hivyo, maombi yake hutokana na chemchemi ya nguvu na yakini, na azma yake huwa madhubuti na imara sana. Na hatimaye kwa kushuhudia neema za Mungu, nuru ya yakini huingia ndani mwake kwa nguvu sana na dhati yake yateketea kabisa, na kwa kutafakari adhama na kudura ya Mungu kwa wingi moyo wake unakuwa nyumba ya Mungu. Na kama vile roho ya mtu huwa haitengani kamwe na mwili wake akiwa mzima, ndivyo ambavyo yakini iliyoingia ndani yake kutoka kwa Mungu Mweza Jalali, haitengani naye katu. Na saa zote roho safi yadumu kuchemka ndani mwake na kwa kufundishwa na roho ile safi husema, na elimu ya ndani na maarifa hutoka kutoka ndani mwake. Na hema la adhama ya Mungu Mwenye heshima na enzi wakati wote linadumu kukita moyoni mwake. Na ladha ya yakini, ukweli na mapenzi hutiririka kila wakati ndani mwake kama maji ambayo kwayo kila kiungo chake kinaonekana kimetosheka. Utoshelevu wa pekee hushuhudiwa machoni mwake, nuru ya pekee ya utoshelevu yang'ara pajini pake; na huhisika kunyesha mvua ya mapenzi usoni pake; na ulimi pia unapata hadhi

kamili ya utoshelevu wa nuru ile. Kadhalika, viungo vyote vyaonekana vimechangamka kama vile baada ya kunyesha mvua ya majira ya kuchipua, ubichi waonekana katika matawi ya miti, majani, maua na matunda. Lakini mtu asiyeteremshiwa roho hiyo wala hakujaliwa utoshelevu huo, mwili wake wote huwa kama jifu, na utoshelevu huu na ubichi na uchangamfu, ambao kalamu haiwezi kueleza, hauwezi kupewa moyo ule uliokufa ambao haukutoshelezwa na chemchemi ya nuru ya yakini, bali unanuka vibaya sana. Lakini mtu aliyepewa nuru hii na aliyebubujikiwa chemchemi hii ndani mwake, alama moja kati ya alama zake ni hii kwamba wakati wote moyo wake unataka kwamba katika kila jambo, katika kila kauli na katika kila amali apate nguvu kutoka kwa Mungu; mumo humo mlipo ladha yake na humo humo anaona raha; hawezi kuishi bila hii. Na maneno yaliyopangwa katika Neno la Mungu kwa kupata nguvu ni yale yale yanayotambulika kwa jina la *Istighfar* – kuomba ghofira.

**Maana ya kweli na halisi ya *Istighfar* ni** kumwomba Mungu kwamba udhaifu wowote wa kibinadamu usidhihirike, na Mungu Aisaidie tabia na Aiingize ndani ya eneo la himaya na nusura Yake. Neno hili limetokana na غَفْر – *ghafr* – linalomaanisha kufunika. Basi, maana yake ni hii kwamba Mungu kwa nguvu yake Afunike unyonge wa tabia ya mwenye kuomba ghofira. Lakini

baada yake, kwa watu wa kawaida maana ya neno hili imepanuliwa zaidi, na pia umechukuliwa muradi wake kwamba Mungu Afunike dhambi iliyoisha tendeka. Lakini maana hasa na ya kweli ni hii tu kwamba Mungu kwa nguvu ya uungu wake Amlinde na unyonge wa tabia yake anayeomba ghofira na Ampe nguvu kutoka kwa nguvu Yake na Amwelimishe kwa elimu Yake na Amjalie nuru kwa nuru Yake. Kwani, Mungu baada ya kumwumba mwanadamu Hakutengana naye, bali kama vile Yu Mwumbaji wa mwanadamu na Mwumbaji wa nguvu zake zote za ndani na za nje, kadhalika Yu Mhifadhi wa milele (*Kayyum*) pia wa mtu, yaani Alichoumba Anakihifadhi pia kwa msaada wake. Basi, Mungu Aitwapo Mhifadhi wa milele pia, yaani Mhifadi wa mahuluku kwa msaada wake. Kwa hiyo, yamlazimu mtu kwamba kama vile alivyozaliwa kwa uumbaji wa Mungu, ndivyo ambavyo ahifadhi sura ya kuzaliwa kwake isiharibike kupitia uhifadhi wa Mungu, kwani uumbaji wa Mungu ulimfanyia mwanadmu hisani hii kwamba ulimwumba kwa sura ya Mungu. Kadhalika himaya ya milele ya Mungu ilitaka isiache kuchafuka na kuharibika sura takatifu ya kibinadmu iliyofanyizwa na mikono miwili ya Mungu, kwa hiyo mwanadamu akafundishwa kwamba kwa *istighfar* aombe nguvu ya uhifadhi Wake. Basi, kama dhambi isingekuwa duniani, hata hivyo *istighfar* ingekuwepo, kwani *istighfar* ndiyo kwa hakika

kwa shabaha hii kwamba jengo la ubinadamu ambalo uumbaji wa Mungu ulijenga, jengo hilo lisipate kubomboka na likae imara. Na bila msaada wa Mugnu haiyumkini kwa kitu chochote kubaki. Basi, hii ilikuwa haja ya asili kwa mwanadamu ambayo kwa ajili yake imeagizwa kufanya *istighfar,* na kwenye hii hii imeashiriwa katika Kurani Tukufu kwamba ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ[9] . Yaani, Mwenyezi Mungu ndiye Apasaye kuabudiwa, kwani Yeye ndiye Ahuishaye na kwa msaada wake mtu anaweza kubaki hai. Yaani kudhihirika kwa mtu kulihitaji Mwumbaji na Mhifadhi, ili Mwumbaji Amwumbe na Mhifadhi Amhifadhi asiharibike, kwa hiyo Mungu ndiye Mwumbaji pia na Mhifadhi wa milele vilevile. Na mtu alipoishaumbika, hapo kazi ya uumbaji imekwisha, lakini kazi ya uhifadhi ni ya kudumu, kwa hiyo haja ya *istighfar* ikatokea. Ilmuradi, kwa kila sifa ya Mungu kuna baraka. Basi, kwa kupata baraka ya sifa ya uhifadhi kuendelea, kufanya *istighfar* kumeashiriwa katika aya hii ya Sura Al-Faatiha: إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ إِيَّاكَ نَسْتَعِينُ[10] , yaani twakuabudu Wewe tu na twakuomba msaada ili kwamba uhifadhi na ulezi wako utusaidie na kutulinda tusikwae, ili isije udhaifu kujitokeza na tusiweze kufanya ibada.

---

[9] Sura Al-Baqara 2:256

[10] Sura Al-Faatiha 1:5

Kutokana na maelezo hayo yote ni dhahiri kwamba maana halisi ya ombi la *istighfar* siyo kwamba hilo lafanywa kwa sababu haki fulani imepotea, bali ni kwa utashi huu kwamba haki yoyote isipotee. Na asili ya kibinadamu ikijiona dhaifu, kitabia huomba nguvu kutoka kwa Mungu, kama vile mtoto amwombavyo mama maziwa. Basi, kama vile tangu mwanzo Mungu Alivyomjalia mtu ulimi, macho, moyo, masikio na kadhalika, ndivyo Alivyomjalia toka mwanzo hamu pia ya kufanya *istighfar* na kumfahamisha kwamba kwa uwepo wake yeye anahitaji kusaidiwa na Mungu. Kwenye hii hii yaashiria aya hii: وَ اسۡتَغۡفِرۡ لِذَنۡۢبِکَ وَ لِلۡمُؤۡمِنِیۡنَ وَ الۡمُؤۡمِنٰتِ[11] , yaani Mwombe Mungu Ahifadhi asili yako na udhaifu wako wa ubinadamu, na aipe asili yako nguvu kutoka Kwake ili unyonge huo usidhihirike. Na kadhalika uendelee kuwaombea wanaume na wanawake waliokuamini dua kiuombezi ili wasalimike na adhabu ya makosa wanayopata kutenda kwa sababu ya udhaifu wa kitabia, na pia maisha yao ya baadaye yasalimike na dhambi. Aya hii yajumuisha hekima ya hali ya juu ya umaasumu na uombezi, na hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba mtu anaweza kufikia daraja ya hali ya juu ya umaasumu na cheo cha uombezi adumupo kuomba muda wote kwa kuzuia udhaifu wake, na vilevile kwa kuwaokoa wengine

[11] Sura Muhammad 47:20

katika sumu ya dhambi, na kavutia nguvu ya Mungu kwa vilio, na kisha anataka wengine pia wapate hadhi katika nguvu hiyo, wanaoungana naye kwa kupitia imani. Mtu maasumu anahitaji kuomba nguvu kutoka kwa Mungu kwani asili ya kibinadmu yenyewe haina ukamilifu wowote, bali kila wakati yapata ukamilifu kutoka kwa Mungu; na haina yenyewe nguvu yoyote, bali kila wakati hupata nguvu kutoka kwa Mungu; na yenyewe haina nuru kamili, bali nuru inaishukia kutoka kwa Mungu. Siri yenyewe iliyomo humo ni kwamba tabia kamilifu hupewa mvuto ili iweze kujivutia nguvu ya juu, lakini hazina ya nguvu ni Mungu Mwenyewe tu. Katika hazina hiyo Malaika pia hujivutia nguvu, na kadhalika mtu mkamilifu pia hujivutia nguvu ya umaasumu na fadhili kutoka katika chemchemi hii ya nguvu kwa njia ya 'bomba' la uabudiwaji. Kwa hiyo, miongoni mwa wanadamu, maasumu kamili ni yule anayejivutia nguvu ya Mungu kwa *istighfar* na kwa mvuto huu hudumisha saa zote unyenyekevu na kilio ili nuru iendelee kumshukia. Na twaweza kuushabihisha moyo kama huo na nyumba ambayo milango yake ya upande wa mashariki na magharibi na ya kila upande yatazamana na jua, hivyo kila wakati mwanga wa jua unaiingia. Lakini, mtu asiyemwomba Mungu nguvu, yu kama chumba kidogo ambacho milango yake imefungwa kwa pande zote nne, usimoweza mwanga kuingia hata kidogo. Basi, *istighfar* ni

kitu gani? Ni kama ala ile ambayo kwa njia yake nguvu inateremka. Siri yote ya tauhidi yafungamana na msingi huu kwamba sifa ya umaasumu isichukuliwe kama mali ya kudumu ya mtu, bali kwa kujipatia huo Mungu tu afahamike kuwa chemchemi. Dhati ya Mwenyezi Mungu kimfano yashabihiana na moyo ulio bohari la damu safi, na *istighfar* ya mtu mkamilifu ni kama vena na arteri zinazoungana na moyo na kuvutia kutoka humo damu safi na kuvigawia viungo vyote vinavyohitaji damu.

## Tofauti Kati ya *Dhamb* (Udhaifu) na Uhalifu

Ni kosa kabisa kusema kwamba katika aya[12] وَ اسْتَغْفِرْ لِذَنْبِكَ kuna neno ذَنْب – *dhamb* – linalomaanisha dhambi, kwani kati ya ذنب – *dhamb* – na uhalifu kuna tofauti. Neno uhalifu daima hutumika kwa dhambi inayostahiki adhabu; lakini neno *dhamb* hutumika kwa udhaifu pia wa kibinadamu, kwa hiyo kuwahusu Manabii, kwa udhaifu wa kibinadamu neno *dhamb* limetumika, lakini neno uhalifu halikutumika; na katika kitabu cha Mungu, nabii yeyote hakuitwa mhalifu. Na tena katika Kitabu cha Mungu, yaani katika Kurani Tukufu, kwa mhalifu kuna onyo la jahanamu, yaani ahadi kutoka kwa Mungu kwamba atatupwa Motoni – lakini, hakuna onyo kwa مُذْنِبٌ (mwenye *dhamb*) – kama Mwenyezi Mungu Asemavyo:

---

[12] Sura Muhammad 47:20

مَنْ يَّاْتِ رَبَّهٗ مُجْرِمًا فَاِنَّ لَهٗ جَهَنَّمَ لَا يَمُوْتُ فِيْهَا وَلَا يَحْيٰى[13], yaani mtu atakayemfikia Mungu akiwa mhalifu, adhabu yake ni jahanamu, humo hatakufa wala hataishi. Basi sehemu hii Mungu Amesema ***mujriman*** sio ***mudhuniban,*** kwani katika baadhi ya hali maasumu pia anaweza kuitwa ***mudhnib***, lakini hawezi kusemwa ***mujrim***. Ipo dalili nyingine juu yake, nayo ni kwamba kuna aya hii katika Sura Aali 'Imraan وَ اِذْ اَخَذَ اللّٰهُ مِيْثَاقَ النَّبِيّٖنَ لَمَاۤ اٰتَيْتُكُمْ مِّنْ كِتٰبٍ وَّ حِكْمَةٍ ثُمَّ جَآءَكُمْ رَسُوْلٌ مُّصَدِّقٌ لِّمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهٖ وَ لَتَنْصُرُنَّهٗ ؕ قَالَ ءَاَقْرَرْتُمْ وَ اَخَذْتُمْ عَلٰى ذٰلِكُمْ اِصْرِيْ ؕ قَالُوْۤا اَقْرَرْنَا[14]. Kwa nususi wazi ya aya hii imethibitika kwamba Manabii wote akiwemo humo Hadhrat Masihi[as] waliamrishwa wamwamini Mtume Mtukufu[saw], nao wakakiri kwamba tumeamini, na kisha inaposomwa aya[15] وَ اسْتَغْفِرْ لِذَنْۢبِكَ وَ لِلْمُؤْمِنِيْنَ وَ الْمُؤْمِنٰتِ pamoja na aya hiyo, na ***Dhamb*** ichukuliwe kumaanisha uhalifu – Mungu apishe mbali – hapo Hadhrat Masihi[as] pia sawa na aya hii atakuwa mhalifu, kwani yeye pia sawa na aya hii yupo miongoni mwa waaminio waliomwamini Mtume Mtukufu[saw]. Basi, bila shaka akawa ***mudhnib***. Wakristo wanapaswa kuzingatia sehemu hii. Basi, kwa aya hizi imethibitika waziwazi kabisa kwamba hapa ***Dhamb*** halimaanishi uhalifu, bali udhaifu wa kibinadamu umeitwa ***Dhamb*** ambalo halipaswi kulaumiwa. Na hakuna

---

[13] Sura Twaa Haa 20:75

[14] Sura Aali 'Imraan 3:82

[15] Sura Muhammad 47:20

budi kwa asili ya mahuluku kwamba udhaifu huu uwepo ndani yake. Na Ameuita udhaifu huu *dhamb,* kwani katika asili ya mwanadamu, kitabia, kasoro hii na upungufu huu upo ili muda wote amhitaji Mungu, na ili kwa kuushinda udhaifu huu wakati wote aendelee kumwomba Mungu nguvu. Na hakuna shaka kwamba udhaifu wa kibinadamu ni kitu ambacho bila kupata nguvu ya Mungu matokeo yake ni dhambi tu. Basi, kitu kinachowasilisha kwenye dhambi chaitwa dhambi kiistiara. Na katika matumizi ya lugha yajulikana kwamba mambo yanayosababisha baadhi ya maradhi, pengine yaitwa kuwa maradhi yenyewe hayo. Basi, udhaifu wa tabia pia ni maradhi ambayo dawa yake ni *istighfar*.

Ilmuradi, Kitabu cha Mungu kimetaja udhaifu wa ubinadamu kuwa *dhamb*, na kimeshuhudia kwamba ndani mwa mwanadamu mna udhaifu wa kiasili, kama Mungu Asemavyo: خُلِقَ الْإِنْسَانُ ضَعِيفًا[16], yaani mwanadamu ameumbwa dhaifu. Huu huu ndio udhaifu usiposaidiwa na nguvu ya Mungu basi husababisha dhambi za aina aina. Basi, uhakika wa *istighfar* ni huu kwamba wakati wote na saa zote msaada uombwe kutoka kwa Mungu, na Aombwe kwamba udhaifu wa ubinadamu – ulio *dhamb* ya ubinadamu – usidhihirike. Basi, kudumu kufanya *istighfaar* ni dalili ya kushinda *dhamb,* nayo haikuweza

[16] Sura An-Nisaa 4:29

kudhihiri; nuru ya Mungu ikashuka na kuishinda. Hapa yapasa kukumbuka kwamba neno la *istighfar* limetokana na غَفر (*ghafr*) na maana yake halisi ni kufunika na kusetiri, yaani kuomba kwamba udhaifu wa ubinadamu usilete hasara kwa kudhihiri na ubaki kufunikika. Kwani, kwa vile mtu si Mungu wala hawezi kujitegemea bila Mungu, kwa hiyo yu kama mtoto anayemhitaji mama yake kwa kila hatua ili amhifadhi kuanguka na amlinde kujikwaa. Kadhalika, mtu huyu pia kwa kila hatua humhitaji Mungu ili Amlinde na kujikwaa na kuteleza. Basi, *istighfar* ndiyo tiba yake.

Na pengine neno hili lapanuliwa maana yake na kutumika kwa wale watu pia ambao wanapata kutenda dhambi, na hapo *istighfar* inamaanisha kuwa Mungu Alinde na adhabu ya dhambi iliyotendeka. Lakini maana hii ya pili haisihi wala haifai kwa watu waliomkaribia Mungu, kwani Mungu huwa Amewadhihirishia mapema kwamba hawataadhibiwa, na watajaliwa daraja za juu Peponi na watakalishwa mapajani mwa rehema ya Mungu. Si mara moja bali mara mia kadhaa wanapewa ahadi kama hizo, na waonyeshwa Pepo. Basi kama wakifanya *istighfar* kwa maana hii kwamba wasiingie Motoni kwa sababu ya madhambi yao, basi *istighfar* kama hiyo itakuwa dhambi kwao kwamba hawana yakini ya ahadi za Mungu na wanajifikiria wako mbali na rehema ya

Mungu. Kisha mtu ambaye Mwenyezi Mungu Aseme kumhusu yeye وَ مَآ اَرۡسَلۡنٰكَ اِلَّا رَحۡمَةً لِّلۡعٰلَمِيۡنَ[17] yaani kwa dunia nzima tulikutuma kuwa rehema, nawe u rehema tupu, kama huyo yuashuku kujihusu kwamba nitajaliwa rehema ya Mungu au la, hapo atasababishaje kuwa rehema kwa wengine.

Karina hizo zote zinawahakikishia wazi watu wanaofikiria kwa uadilifu kwamba maana ya pili ya *istighfar* kumnasibishia Mtume Mtukufu^saw ni hatia kubwa na shari. Kwa hakika alama ya kwanza ya maasumu ni kwamba ajishughulishe katika *istighfar* zaidi kuliko wote, na wakati wote; na katika hali zote aombe nguvu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kujilinda katika udhaifu wa ubinadamu – jambo liitwalo *istighfar* kwa maneno mengine. Kwani, kama mtoto akitembea saa zote kwa kushika mkono wa mama na haoni sawa kuwa mbali na mama hata kwa sekunde moja, bila shaka mtoto huyo atasalimika kujikwaa. Lakini mtoto yule anayetembea akitengana na mama na pengine mwenyewe anapanda ngazi ya hatari, na pengine anashuka kutoka ngazi ya hatari, lazima siku moja ataanguka, na ataanguka vibaya sana. Basi, kama vile kwa mtoto mwenye bahati njema ilivyo afadhali asitengane kamwe na mama yake mpendwa wala kamwe asitengane na mapajani mwake,

[17] Sura Al-Ambiyaa 21:108

wala asiachane naye, ndivyo inavyokuwa tabia ya watakatifu kwamba wanakaa kizingitini pa Mungu kama vile watoto mapajani mwa mama. Na kama mtoto anavyotimiza haja zake zote kwa nguvu ya mama, na mtoto mwingine anapopingana naye au mbwa anapomkabili au hofu nyingine inapotokea au anapojikuta penye kutelezesha, mara anamwita mamaye ili haraka amkimbilie na kumlinda na balaa ile, ndivyo hivyo inavyokuwa hali ya watoto hao wa kiroho kwamba wakimfahamu Mola wao kabisa kama mama, wanaona nguvu Zake ni kama bohari lao na huendelea kuomba nguvu Zake kila wakati na kila saa. Na kama vile mtoto mchanga wakati wa njaa anavyoweka midomo yake titini pa mamake na kwa mvuto wake wa kitabia anataka kujivutia maziwa, na mama anapohisi kwamba midomo myororo ya mtoto huyo akilia imeligusa titi lake, maziwa yake kitabia yabubujika na kuanguka kinywani mwa mtoto. Basi, kanuni hii hii pia ni kwa ajili ya watoto wanaotaka maziwa ya kiroho.

## Haja ya Uombezi

Yumkini, hapa mtu aulize pia kwamba kwa nini mwanadamu anahitaji uombezi, na kwa nini haijuzu kwamba mtu kwa kutubu na kuomba ghofira moja kwa moja apate msamaha kutoka kwa Mungu. Kanuni ya ulimwengu yenyewe yatoa jibu la swali hili. Kwani,

imekubaliwa na hakuna awezaye kupinga kwamba kanuni ya kuzaa kwa binadamu, bali wanyama wote, yaendelea kwa uombezi (shfa'at) tu. Kwani, tumeshaandika sasa hivi kwamba neno la شَفَاعَت limetokana na شَفْع linalomaanisha jozi, basi yaweza kuwa shaka gani kwamba baraka zote za kuzaa zimepatikana na zaendelea kupatikana kutokana na 'jozi'. Hulka, nguvu na sura ya mtu mmoja hudhihirika katika mtu mwingine kwa njia hii hii, yaani ndiyo matokeo ya muungano. Kadhalika, mnyama mmoja huzaliwa na mwingine, kwa mfano mbuzi, ng'ombe, punda na wengineo, nguvu zote zaingia kutoka mnyama mmoja katika mnyama mwingine, hayo pia kwa kweli ni matokeo ya kuwa muungano. Basi, muungano huu huu unapochukuliwa kwa maana hii kwamba mpungufu mmoja akiungana kiroho na mkamilifu anapopata tiba ya udhaifu wake kutokana na roho yake na kusalimika na jazba za nafsi, basi muungano huu ndio waitwa uombezi. Mathalan, mwezi ukitazamana na jua, hupata umoja nalo na muungano wa aina fulani, papo hapo hujipatia nuru iliyopo katika jua. Na kwa kuwa muungano huu inaoupata mioyo iliyojaa huba kutoka kwa Manabii, una mnasaba na muungano huu wa kimwili ambao, kwa mfano, Zaid anao na baba yake, kwa hiyo wajipatiao baraka hii ya kiroho nao pia huitwa mbele ya Mungu wazao; na wenye kupata kikamilifu kuzaliwa huku, hupata sura, hulka na baraka zile zinazokuwa

katika Manabii. Basi, kwa kweli huo ndio uhakika wa uombezi. Na kama vile ilivyolazimu kwa kuungana kimwili kwamba hali ya wazao yaafikiana na hali ya mtu ambaye muungano ulifanywa naye, ndivyo ilivyo sifa ya muungano wa kiroho pia. Ilmuradi, uhakika wa uombezi ndio huu kwamba kanuni ya Mungu, kimwili na kiroho, tangu kale ndiyo kwamba baraka zote zinapatikana kwa muungano tu; tofauti ni hii tu kwamba aina moja imeitwa شَفْع (jozi) na aina ya pili imeitwa شَفَاعَت (uombezi). Na kama vile mtu anavyohitaji شَفْع kwa kudumisha kuzaa ndivyo hivyo kwa kudumisha silsila ya kiroho huhitaji شَفَاعَت . Na Neno la Mungu limeeleza aina zote mbili, kama vile sehemu fulani katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Alivyosema kwamba Mungu Alimwumba Adamu pamoja na mwenzake, kisha kutokana na hao wawili akaumba watu wengi, wanaume kwa wanawake. Kadhalika Akasema kwamba Mungu Akaumba juu ya ardhi Khalifa Wake aliyekuwa Adamu mwenye roho ya Mungu ndani mwake, kisha nuru ile kutoka Adamu ikaendelea kuhamia kwenye Manabii wengine. Na Ibrahimu, Isihaka, Ismaili, Yakubu, Musa, Daudi, Isa na wengineo, wote wakarithi nuru ile mpaka mrithi wa mwisho Nabii wetu[saw] akatumwa. Basi, Manabii hao wote watakatifu jinsi walivyomrithi Adamu sura ya kimwili ndivyo walivyojipatia roho ya Mungu pia kutoka kwake kwa sababu ya Adamu kuwa Khalifa. Kisha

kupitia hao, watu wengine pia waliendelea kurithi katika nyakati mbalimbali.

## Ithibati ya Uombezi wa Mtume Mtukufu[saw] Kutoka Katika Kurani Tukufu

Katika Kurani Tukufu uombezi wa Mtume Mtukufu[saw] umetajwa katika sehemu mbalimbali kama vile katika sehemu fulani Akasema قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِیْ يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ وَ يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ[18] Tafsiri: Sema: Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, ili Mwenyezi Mungu pia Awapendeni na Awaghofirieni madhambi yenu. Sasa angalieni, aya hii inaeleza waziwazi kwamba kufuata nyayo za Mtume Mtukufu[saw], ambako katika sharti zake ni huba, taadhima na utii wa Mtume Mtukufu[saw], natija yake ya lazima ni kwamba mtu anakuwa mpendwa wa Mungu na madhambi yake yasamehewa, yaani ikiwa mtu ameshakula sumu ya dhambi, basi kwa kiuasumu cha huba, utii na ufuasi, athari ya sumu hii yafutika. Na kama vile kwa dawa mtu anavyoweza kupona maradhi, hivyo ndivyo mtu anavyoondokewa na dhambi. Na kama vile mwanga huondoa giza na kiuasumu hufuta athari ya sumu, na moto huunguza, ndivyo hivyo inavyokuwa athari ya utii na huba ya kweli. Angalieni, jinsi moto huchoma mara moja, hivyo ndivyo wema wenye jazba

[18] Srua Aali 'Imraan 3:32

unaofanywa kwa kudhihirisha tu utukufu wa Mungu, huwa kama moto kwa kuchoma takataka za madhambi. Mtu anapomwamini Nabii wetu Mtukufu[saw] kwa moyo wa kweli na akikubali adhama na utukufu wake anamfuata kwa ikhlasi kamili, huba na utii, hata kwamba kwa utii kamili anafikia daraja ya kujipoteza, basi kwa uhusiano huu imara unaojengeka naye, nuru ile ya Mungu inayomshukia Mtume Mtukufu[saw], mtu huyu pia anapata hadhi yake katika hiyo, ndipo kwa vile giza na nuru havipatani, giza lililomo ndani yake huanza kuondoka hata kwamba sehemu yoyote ya giza haibaki ndani mwake. Kisha kwa kujipatia nguvu kutoka katika nuru hii, mema ya hali ya juu hudhihirika toka kwake, na katika kila kiungo chake nuru ya huba ya Mungu inang'ara, ndipo giza la ndani huondoka kabisa, na kielimu pia nuru huzalika ndani yake na kiamali pia nuru huzalika. Hatimaye, kwa mkusanyiko wa nuru hizi, giza la dhambi huuhama moyo wake. Hii ni dhahiri kwamba nuru na giza haviwezi kujumuika sehemu moja, hivyo nuru ya imani na giza la dhambi pia haviwezi kujumuika mahalli pamoja. Na ikiwa dhambi yoyote haikutendwa na mtu wa aina hii kwa bahati, basi anapata faida hii kwa ufuasi huu kwamba kwa siku zijazo anaondolewa mbali nguvu ya kutenda dhambi na hupata shauku ya kutenda mema kama vile Mwenyezi Mungu anavyosema kuhusu hiyo katika Kurani Tukufu حَبَّبَ اِلَيْكُمُ الْاِيْمَانَ وَ زَيَّنَهٗ فِیْ قُلُوْبِكُمْ وَ كَرَّهَ اِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَ

الْفُسُوقَ وَ الْعِصْيَانَ[19], kwamba Mungu Akiwashushieni roho takatifu Amewaelekezeni kwenye kila wema na amefanya makuruhu kufuru, ufasiki na uasi machoni penu.

Lakini kama lizuke hapa swali kwamba nuru ile apewayo mfuasi kupitia Nabii[as] inayofutilia mbali jazba za kutenda dhambi ni kitu gani, basi jibu lake ni kwamba nuru hiyo ndiyo maarifa matakatifu yasiyo na giza lolote la shaka na wasiwasi; nayo ndiyo huba tukufu isiyo na tamaa ya kinafsi; ni ladha tukufu izidiyo ladha zote isiyo na uchafu wowote; ni mvuto wenye nguvu ambao hakuna mvuto mwingine uushindao; ni kiuasumu chenye athari kubwa kinachoua sumu zote za ndani. Hivi ni vitu vitano viteremkiavyo moyoni mwa mfuasi wa kweli, kama nuru pamoja na Roho Mtakatifu. Basi, moyo kama huo sio kwamba hujitenga na dhambi, bali kiasili huichukia pia. Kueleza nguvu ya kila kimoja cha vitu hivyo vitano kwahitaji maelezo marefu, lakini kuzieleza kiasi fulani sifa za maarifa matakatifu kunatosha kwa kuelewa uhakika huu kwamba namna gani maarifa matakatifu yazuia kutenda dhambi.

Hii ni dhahiri kwamba mwanadamu, bali mnyama pia, baada ya kupata elimu sahihi na ya yakini ya kitu chenye madhara hawezi kusogea karibu nacho. Mwizi akijua

[19] Srua Al-Hujuraat 49:8

kwamba pale anapotaka kutoboa ukuta wa nyumba kwa kuibia, kundi la watu linavizia litakalonikamata katika hali ya kutoboa ukuta, basi kamwe hawezi kujasiri kutoboa hapo. Bali, hata kama ndege pia akitambua kwamba punje hizi chache nilizomwagiwa uwanjani, chini yake upo mtego, basi haji karibu na punje zile. Kadhalika kama, kwa mfano, chakula kizuri, kinono, kimepikwa, lakini mtu akijua kuna sumu ndani yake, haelekei kula chakula hicho. Basi, kwa kutazama hayo yote yadhihirika kwamba mtu apatapo elimu kamili kuhusu kitu cha kuudhi na kudhuru, kamwe hakielekei kitu hicho, bali hukimbia asikione sura yake. Kwa hiyo, yafaa kukubali kwamba ikiwa mwanadamu apate kuelimika kwa njia yoyote kwamba dhambi ni sumu ya kuua inayoua mara moja, basi bila shaka baada ya elimu hii mtu hatatenda dhambi katu. Lakini hapa panazuka swali hili kwamba njia ile ni ipi? Je, akili yaweza kuwa njia hiyo? Basi, jibu lake ni kwamba akili haiwezi kamwe kuwa njia kamili mpaka awepo msaidizi yeyote wa kimbingu. Kwani yakini hii moyoni kwamba kwa dhambi kuna adhabu ambayo mtu hawezi kuikimbia yaweza kwa ukamilifu ijulikanapo kikamilifu kwamba Mungu Yupo Awezaye kutoa adhabu ya dhambi. Lakini mwenye akili pekee asiyepata nuru kutoka mbinguni, hawezi kuwa na yakini kikamilfu juu ya Mwenyezi Mungu, kwani hajasikia mwenyewe maneno ya Mungu wala hakuona uso Wake. Hivyo, yeye anaweza

kupata elimu kiasi hiki tu – sharti akitafakari juu ya viumbe vya mbingu na ardhi aweze kufikia natija sahihi – kwamba yapasa awepo mtengenezaji wa vitu hivi vyote, lakini hawezi kufikia elimu ya yakini kabisa kwamba mtengenezaji huyo yupo pia. Na ni dhahiri kwamba kati ya 'kupaswa kuwepo' na 'kuwepo' kuna tofauti kubwa. Yaani, mtu ambaye elimu yake inaishia tu kwenye 'yapasa kuwepo', basi zaidi ya hapo analo giza tu mbele ya macho yake. Huyo sawa na elimu yake siye katu kama mtu yule asiyesema tu kuhusu mtengenezaji wa kweli kwamba apaswa kuwepo, bali kwa ushahidi wa nuru ile aliyopewa anatambua vilevile kwamba Huyo Yupo pia. Na siyo hii tu kwamba anashuhudia uwepo wa Mungu kwa nuru ya kimbingu tu, bali kwa mwongozo wa nuru ile ya kimbingu, nguvu zake pia za akili na fahamu zinafanywa kuwa kali kiasi hiki kwamba haja yake ya kukisia pia huwa bora ya hali ya juu. Basi, huyo ana yakini juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu kwa nguvu maradufu. Hapa muradi wa nuru ya kimbingu ni kwamba huyo anabahatika kwamba Mwenyezi Mungu Anaongea naye kwa yakini, au Huwa na uhusiano mkubwa na Anayeongea naye. Na maongezi ya Mungu hayamaanishi kwamba yeye anadai kupokea ufunuo kwa kudhani kama watu wa kawaida, kwani ufunuo wa dhana si chochote, bali ni kinyume na akili pia. Kwa hakika maana yake ni kwamba ufunuo huo kwa kweli huwa kwa yakini kabisa kabisa wahyi mtakatifu na

mkamilfu wa Mwenyezi Mungu ambao hakuna budi kuwa na ishara za kimbingu pamoja nao. Na wahyi huo huwa na shani na adhama kubwa sana, na kwa maneno yake yenye haiba na ladha huingia moyoni kama msumari wa chuma cha pua na huwa na muhuri mwangavu wa ishara za Mungu na alama zisizo za kawadia. Na ili kupata yakini kamili juu ya Mungu, mtu kwanza kabisa anahitaji kwamba abarikiwe mwenyewe na wahyi kama huu, au awe na uhusiano imara na aliyebarikiwa nao, anayejivutia mioyo kwa athari yake ya kiroho. Kwa hiyo, kila dini isiyoweza kutoa wahyi mpya mpya ulio na ishara zilizo hai, ni kama mifupa iliyochakaa ambayo udongo umeifanya kama udongo. Na haiyumkini kwa dini kama hiyo kuweza kuleta mabadiliko yoyote ya kweli; na waifahariao wanaweza kuwa wale tu wanaopenda kufuata nayo za baba zao; na hamna rohoni mwao hamu ya kutafuta ukweli wala hawana shauku ya hamu kama hiyo, bali kwa kuupenda uadui mkali na upotevu hali yao ya ndani inabadilika kabisa. Hawajali kutafuta njia ya kuweza kumwamini Mungu kwa yakini na kwamba Mungu Huyo anapaswa kuwa na sifa zipi Awezaye kuaminika kwa yakini; na ni yepi mambo yanayoweza kuyakinisha uwepo wa Mwenyezi Mungu; na alama za yakini ni zipi zinazokuwa alama bainifu kwa mwenye kuyakini. Kumbukeni, hata kama dini fulani iliyo na hoja ya kiakili kiasi fulani na inayo sifa pia ya ustaarabu na adabu njema,

lakini kwa kiasi hicho tu haitasemwa kwamba dini hiyo inafikisha kwenye daraja ya yakini kuhusu uwepo wa Mwenyezi Mungu na sifa Zake, bali dini zote za ulimwengu ni upuuzi mtupu zisizofaa, mbovu, zisizo na uhai na zimekufa mpaka zimfikishie mtafutaji kwenye chemchemi safi ya yakini.

Ni masikitiko kwamba watu wengi hawaelewi kwamba ni kitu gani kuyakini uwepo wa Mungu, dhati Yake, adhama na kudura Yake na sifa Zake zingine njema. Na kama kwa masikitiko juu ya hali yao idhihirishwe rai hii kwamba hao hawanayo chemchemi safi ya yakini, hivyo hawanao utakaso wa kweli pia upatikanao baada ya yakini, basi wanakasirikia sana, na wakihamaki husema, je hatuna yakini juu ya Mungu, je hatumwamini Yeye? Jibu la hayo yote ni kwamba kwa hakika ninyi hamna yakini juu ya Mungu wala hammwamini Yeye. Ni masikitiko kuwa hawafahamu kwamba katika shimo wanamoyakini mna nyoka mwenye sumu hawaingizi mle mkono wao kwani wanaona humo mna hilaki yao, lakini wanajasiri kutenda kila dhambi. Hawali sumu ya kuua kwani wanajua watakufa, lakini wanatenda maasi makubwa ya kutisha; bali achilia mbali yakini, hata kwa dhana imara pia hawatendi kitendo wanachodhania kwamba kitadhuru. Kwa mfano, hawapendi kulala chini ya paa ambalo boriti yake imepasuka kiasi fulani; hawataki kukaa

kijijini mnamotokea kipindupindu au tauni. Basi, kuna sababu gani kwamba juu ya madai yao ya kuwa na yakini wanavunja amri za Mwenyezi Mungu. Basi, fahamuni kwa yakini ukweli huu kwamba kwa hakika hao hawana yakini, bali hawana hata dhana imara pia kwamba Yupo Mweza Anayeweza kuhilikisha mara moja.

## Mungu wa Wakristo

Siku hizi maradhi haya hayalihusu tu kundi moja mahususi, bali kama vile yalivyopo katika Wakristo, ndivyo yalivyopo katika Waislamu pia, na watu wa mashariki pia sawa na hali wamepata sehemu yake kama watu wa magharibi. Tofauti baina ya Waislamu na Wakristo ni hii kwamba Waislamu wameshamghafilikia Mungu Mweza kwa uzembe wao; hata hivyo daima Mungu anawadhihirishia nuru Yake na katika kila zama Anawavutia Kwake, na watu wema wengi wanapata hadhi ya nuru hii. Lakini Wakristo tangu muda mrefu wamepotewa na Mungu Yule Ambaye kwa sababu ya kuwa na yakini juu yake mabadiliko matakatifu hupatikana, na kwa kufikiria adhama na utukufu wake, huzalika kwa hakika chuki ya kweli dhidi ya dhambi. Na watu hao badala ya Mzima wa milele na Mhifadhi wanamchukulia mtu mnyonge, aliye mwana wa Mariamu, aitwaye Yesu, kuwa Mungu ilihali yeye hawezi kuitikia maombi wala mwenyewe hawezi kusema na yeyote, wala

hawezi kudhihirisha adhama na kudura yake yoyote. Basi, kumpitia yeye utakaso wa kweli utapatikanaje? Mifano ya kudura yake iliyoandikwa vitabuni ni hii tu kwamba alipata kusumbuliwa na Wayahudi, dua yake ya usiku kucha haikukubaliwa, mamaye akafanyiwa shutuma ya kuaibisha, lakini yeye hakuweza kumtetea kwa mng'ao wa Kiungu. Miujiza yake, ikikubaliwa kuwa sahihi, hamna ndani yake ubora usiokuwemo katika miujiza ya Manabii wengine, bali miujiza ya Nabii Eliya na kuwahuisha kwake wafu ni kudura kamili inayoshinda miujiza ya Masihi. Kadhalika, ipo baadhi ya miujiza ya Nabii Isaiah pia ambayo kulingana nayo miujiza ya Masihi si kitu chochote. Na matabiri ya Hadhrat Masihi hayana thamani, hata kwamba badala ya kuleta athari nzuri mioyoni yachekesha yakisomwa. Ni matabiri ya aina gani haya kwamba ukame utatokea, matetemeko ya ardhi yatatokea na vita vitapiganwa, ilihali kabla ya matabiri hayo pia hayo yote yalikuwa yanatendeka nchini. Basi, mwenye lubu amwaminije mungu kama huyo. Hivi ni visa vya zamani, Mungu tu Anajua kuna ukweli kiasi gani humo na uongo kiasi gani. Lakini, kwa watu wa zama hizi matatizo yamezidi sana kumwamini mungu mpya ambaye hakuna habari zake hata katika mafundisho ya Wayahudi. Kwani, watu hao hawakuona kwa macho yao wafu kufufuliwa; wala hawakuwashuhudia kwa macho yao wagonjwa kuondokewa na majini, pepo wachafu; wala

hazikutimia ahadi walizoziahidiwa, yaani wakila sumu, haitawadhuru, na wakiuamuru mlima kuondoka mahali pake basi utaondoka mara moja, na wakishika nyoka mikononi mwao, hawatawauma. Kwani, twaona Wakristo wengi wa Ulaya wanakufa wakijiua, sumu inawaathiri mara moja; na achilia mbali mlima, hata kiatu kilichopinduka hawawezi kukiweka sawasawa kwa kukiamrisha tu mpaka watumie mkono wao; na sikuzote wanakufa kwa kuumwa na nyoka na wanyama wengine wenye sumu. Sasa kwa kulijibu ikisemwa kwamba haipasi kuchukua tafsiri sisisi ya aya hizi, bali hapa zina maana ya kimajazi. Mathalan, maana ya sumu ni kwamba wanameza mate ya uchungu – wanazuia hasira, na maana ya nyoka ni kwamba washari hawawezi kuwadhuru. Basi, kabla ya kuzungumzia hizi maana za kimajazi, tunayo haki tuulize wakati huu swali hili kwamba kwa kuwa madai haya yote yaliyotajwa kuhusu ishara – na mara kwa mara Hadhrat Masihi[as] akasema kwamba ishara ninazozionyesha mimi, wafuasi wangu pia wataonyesha ishara hizo – ndizo kwa sura ya kiistiara na kimajazi tu na hazimaanishi ishara zenyewe, basi yathibitika waziwazi kwamba miujiza inayoyanasibishwa kwa Hadhrat Masihi[as], hiyo pia ni kwa sura ya kiistiara. Kwani, Hadhrat Masihi[as] amesema mara kwa mara katika Injili kwamba miujiza ninayoonyesha, miujiza hiyo hiyo wafuasi wangu wa kweli pia wataendelea kuonyesha. Sasa kwa kuwa

wanapoambiwa waonyeshe miujiza kama hiyo, twajibiwa kwamba sehemu hizi hazimaanishi miujiza, bali muradi wake ni hali za kihulka za Wakristo, basi kwa nini isisemwe kwamba miujiza ya Hadhrat Masihi[as] pia yamaanisha mambo kama hayo, siyo miujiza kwa hakika. Ilmuradi, kwa Wakristo, swali hili ni msiba mkubwa, ambalo hawana jibu lake lolote. Sasa, hapa ikitafakariwa zaidi kidogo, basi kwa kweli huu si msiba mmoja, bali ni misiba mitatu: (1) Kwanza ni huu kwamba kauli ya Masihi kwamba miujiza ninayoonyesha, miujiza hiyo bali zaidi ya hiyo wataonyesha wafuasi wangu, jambo hili limethibitika kuwa uongo kabisa. (2) Pili, uongo huu umethibitisha hii pia kwamba Masihi naye hakuonyesha muujiza wowote, kwani ikiwa Masihi alionyesha muujiza wowote, basi ilikuwa lazima wafuasi wa Masihi wangekuwa na uwezo wa kuonyesha miujiza. (3) Wa tatu, hata kama tukikubali jambo hili lisiloweza kuthibitishwa kwamba Masihi akaonyesha miujiza pasipo kujali ibara zile zilizoandikwa katika Injili kwamba 'Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara yoyote', hata hivyo kwa miujiza kama hiyo isiyoizidi miujiza ya Manabii wa zamani, bali ni duni, uungu wa Masihi hauwezi kuthibitika. Basi, wakati uungu wa Masihi ni wa namna hii ambao mtu mwenye akili timamu hawezi kwa vyovyote kupata yakini juu yake, basi uungu kama huo utawezaje kuzuia dhambi. Tumeshaandika awali

kwamba jambo la kwanza kabisa linalozuia dhambi ni yakini juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu, yaani yakini hii kwamba kwa hakika Yupo Mungu Mmoja Anayeadhibu utendaji wa dhambi, lakini kuhusu Masihi yakini kama hiyo iwezeje kupatikana. Ebu, mtu yeyote atuambie kuna tofauti gani baina yake na wale walioishafariki. Sisi, na kila mwenye akili, tunajua vizuri kwamba kati ya Mungu na mahuluku yapaswa kuwepo tofauti bainishi, lakini hapa achilia mbali tofauti bainishi bali tofauti kiasi hiki pia haithibitiki inayoweza kuwapo kati ya mtu mzima na mfu. Ni sikitiko kwamba Wakristo wanapiga makelele kuhakikisha uungu wa Masihi, lakini twaweza kuridhika kwa kiasi hiki tu kwamba wathibitishe kuwa Masihi yu mtu aliye hai. Hatuibugudhii dini yoyote. Ikiwa mwana wa Mariamu yu Mungu, tupo tayari kumkubali kabla ya wengine wote; ikiwa kwa hakika yeye ndiye Mwombezi, twataka tuwe wa kwanza kuamini. Lakini tukubalije batili tupu, upuuzi na uongo. Kama Mungu anapaswa kuwa dhaifu na mnyonge kama alivyo Yesu mwana wa Mariamu, basi hakuna haja hata kidogo ya kumwamini mungu kama huyo, wala kwa vyovyote haiwezi kuwa yakini juu yake. Lakini ikiwa Yesu Masihi ni Mungu ambaye twaweza kumtambua namna Mwenyezi Mungu Alivyoendelea kujitambulisha katika kila zama Yeye Mwenyewe na pia kupitia Manabii, na hata wale pia hawakukosa kumtambua ambao

hawakufikiwa na Vitabu vya kimbingu, basi sisi tupo tayari kumkubali. Kwa hiyo, je yupo mtu juu ya uso wa ardhi ambaye atuonyeshe ishara bainishi yoyote ya Masihi, yaani tuweze kusikia sauti yake na tuweze kuona ishara za uungu wake? Kwani, tumeshaandika mara kwa mara kwamba ikiwa imani iwe ya shaka tu juu ya Mungu wa kweli pia ambaye Yu Mungu kwa hakika, hata hivyo imani kama hiyo haiwezi kuokoa katika madhambi, basi kama mungu wa bandia aliyeendelea kupigwa na Wayahudi akidhaniwa kuwa mungu, dhana hiyo itaokoa katika maradhi gani? Hili ni jambo la yakini kwamba Mungu Yule, Aliye Mungu wa kweli, kumwamini Yeye pia kunaweza kuokoa katika dhambi iwapo imani hiyo iwe imeishafikia daraja ya yakini. Hivyo, kumfanya mtu kuwa Mungu na kutotolea hoja za yakini juu ya uungu wake ni aibu kubwa kiasi gani! Na kwa kweli watu kama hao ni maadui wa ukweli. Siwezi kuelewa kwamba watu hao walikuwa na haja gani ya kufanya kitendo hiki cha aibu, na katika kumwamini Mungu wa azali na abadi wakatazamia hasara zipi zilizoondolewa kwa njia ya mungu huyu wa kubuniwa. Twashuhudia kwamba Mungu Yule Mkweli Aliyedhihiri kwa Adamu, tena kwa Sethi, kisha kwa Nuhu, Ibrahimu, Musa na Manabii wote mpaka kwa Nabii[saw] wetu, Yu hai kwa kudumu, Mzima na Mhifadhi wa milele. Na kama kupitia Manabii katika zama za awali Alivyosema Nipo, ndivyo Asemavyo sasa

pia. Na kama vile Manabii wa zamani wakasikia sauti zake zenye adhama na kuona ishara zake, ndivyo hivyo tusikiavyo sauti na kuona ishara. Na kama vile katika zama za awali Alivyokuwa akisikia na kujibu maombi ya waja wake, hivyo ndivyo sasa pia husikia na kujibu maombi yetu. Na kama wanyofu wa zamani wakapata utakaso wa kweli kwa kumpenda na kuona Uso Wake, hivyo ndivyo tuendeleavyo kujipatia sisi pia. Basi, yule tu atamwacha Huyu Mungu Mwenye nguvu na Mweza atakayekuwa mwenye bahati mbaya sana na kipofu. Tuna yakini kwamba waliofanywa duniani miungu wa bandia kama vile Yesu mwana wa mariamu, Ram Chandar, Krishna, Budha na kadhalika, wamefanywa pasipo dalili yoyote iwayo. Mfano wake ni kama vile mbuzi aitwe kuwa mwanadamu ilihali hasemi wala hawezi kutembea kama binadamu, wala hana sura ya wanadamu, wala hana akili kama wanadamu, wala hana alama yoyote ya ubinadamu. Basi je, mwaweza kumwita mbuzi kuwa mwanadamu ilihali katika mambo mengi mbuzi anashirikiana pia na mwanadamu. Mathalan, mbuzi anakula kama vile mwanadamu hula na mbuzi anakojoa na kujisaidia kama vile mwanadamu anavyofanya. Lakini, je mtu yeyote aweza kutuambia kwamba Masihi au Ram Chandar na wengine wanao ushirikiano wowote maalumu na Mungu unaoweza kuthibitika.

Hakuna sababu yoyote ya kufanywa kwa miungu hao isipokuwa tu kwamba dhidi ya kupunguza hadhi sana ikashikwa njia ya kuzidisha hadhi kupita kiasi. Mathalani, Raja Ravan alipomdhalilisha vibaya sana Raja Ram Chandar na kuwaudhi sana watu wake kwa kumteka mkewe na kumpeleka Lanka, hapo kundi la wasaidizi wa Raja Ram Chandar haraka sana wakamtoa Raja Ravan nje ya kizazi cha wanadamu na wakamfanya Raja Ram Chandar kuwa Parmeshar (Mungu) kwa yakini kamili hata kwamba sasa Mabaniani wote badala ya kutaja jina la Mungu wao, husema *'Ram Ram'*, bali wanaamkiana pia kwa kusema '*Ram Ram*'. Yaonekana kutokana na jambo hili kwamba Wakristo bado hawajapiga chuku kumfanya Yesu kuwa Mungu kadiri waliyopiga chuku Mabaniani kumfanya Ram Chandar kuwa Mungu hata kwamba Mabaniani karibu wakasahau jina la Parmeshar wao, na kila wakati wanatumia '*Ram Ram*' kwa wingi. Basi, kwa sababu ya ghera ile ya kukabiliana na kupiga chuku Raja Ram Chandar amefanywa kuwa Mungu; kwa sababu hizo hizo Yesu mwana wa Mariamu naye pia akafanywa kuwa Mungu. Yaani, kwanza Wayahudi wakorofi wakavumisha kwamba Hadhrat Masihi[as] amezaliwa kwa njia isiyo halali, na wakamtuhumu Hadhrat Mariamu kufanya uzinzi na tena wakamzulia uwongo Bwana Yesu mwenendo wake. Vitabu vichache vya watalaamu wa Kiyahudi tunavyotalii siku hizi, kwa kuvisoma hivyo inaonekana wamepiga

taswira mbaya sana ya maisha ya Bwana Yesu. Vitabu hivi vya wataalamu wa Kiyahudi vinasomwa siku hizi, saa za jioni katika kikao chetu kwa lengo hili tu kwamba Jumuiya yetu ipate kujua ya kuwa siku hizi baadhi ya Mapadri wajinga wanaomshambulia Nabii[saw] wetu maisha yake kwa kumzulia uongo na kumsingizia, basi Bwana Yesu ameshambuliwa viovu zaidi maisha yake kuliko mashambulizi hayo, hata kwamba kuna baadhi ya mashambulizi ambayo aibu na haya yazuia hata kuyaandika pia. Mama yake akatuhumiwa vibaya mno. Kadhalika, baadhi ya nyanya zake yaani Tamar, Rahab na Bathsheba wakalaumiwa kwa tuhuma za uasherati ambazo hata mapadri wanazikubali. Na tuhuma zile ni mbaya zaidi kuliko zote alizoletewa Bwana Yesu kuhusu mienendo yake, na kwamba akadanganya katika kila jambo, na hatimaye jinsi gani, sawa na ahadi ya Torati, Mungu Alivyompa adhabu ya kifo. Maneno haya yote ya dhila, fedheha na tuhuma ndiyo ambayo Mwislamu hawezi kuyasoma bila kukasirika pasipo hiari yake. Basi, Bwana Yesu alipofedheheshwa kiasi hiki kwamba hata akashushwa chini ya daraja ya mwanadamu wa kawaida, hapo kitabia ikabidi kwamba watu waliomwamini Bwana Yesu waelekee, hatua kwa hatua, kupita kiasi katika kumheshimu. Kwa hiyo, watu wenye harara waliopenda shirki hapo kabla hawakuweza kuridhika pasipo kumfanya Bwana Yesu kuwa Mungu, kana kwamba kwa

njia hii wakataka kulipa kisasi cha mashambulizi ya Wayahudi aliyofanyiwa Bwana Yesu kwa ukali sana. Na la ajabu zaidi sana ni kwamba kutokana na zile Injili ambazo kwazo Wakristo wanataka kuthibitisha uungu wa Bwnaa Yesu, kwa njia ya Injili hizo hizo mtaalamu mmoja wa Kiyahudi ametaka kuthibitisha katika kitabu chake kwamba – Mungu Apishe mbali – mtu huyu kwa hakika alikuwa mpenda mambo ya anasa za dunia na alikuwa laghai ambaye hakuonyesha muujiza wowote wala haikutimia bishara yake yoyote. Na ameandika kwamba inayoelezwa katika Injili kwamba Bwana Yesu aliowaonyesha Wayahudi ishara nyingi, kauli hii yabatilika kutoka katika maelezo ya Injili zenyewe. Kwani, yathibitika kwa ushahidi wa Injili kwamba wazee wa kaumu walipokuwa wakimwomba Yesu kuonyesha muujiza, yeye akiwatolea wazee hao matusi machafu alikuwa akisema kwamba hao hawataonyeshwa muujiza wowote. Tena anasema kuwa hata tukiamini kwamba akawaponyesha baadhi ya wagonjwa, basi hii siyo dalili ifaayo kuhakikisha uungu wake, kwani katika zama hizo hizo wapinzani wake pia wakaonyesha miujiza kama hiyo. Basi, je, kwa miujiza ambayo zaidi sana kuliko hiyo Manabii wengine waliendelea kuionyesha, akili yaweza kukubali kwamba uungu wa Yesu utathibitika? Ilimuradi, Wayahudi walipomfedhehesha vikali Bwana Yesu, matokeo yake ya lazima yalikuwa kwamba kufeheheshwa

kupita kiasi sana kulipizwe kwa kumheshimu kupita kiasi. Basi, mafuriko wa kumheshimu Yesu kupita kiasi yalipozuka kwa nguvu ndani ya Wakristo, katika zama hizo hizo msingi ukawekwa kumfanya Bwana Yesu kuwa Mungu. Jambo hili laweza kueleweka vizuri ambapo kwa upande mmoja yatazamwe mashambulizi ya Wayahudi na kwa upande wa pili yaangaliwe kwa makini mambo ya kupiga chuku ya Wakristo kwa kusalimika na mashambulizi hayo. Sasa kwa kuwa vitabu vya Wayahudi pia vimeshachapishwa, na baadhi ya wataalamu walio Wayahudi wamevichapisha kwa Kifransa pia, na kwa Kiingereza vilevile vimechapishwa, kwa hiyo katika siku hizi watafutao haki wamerahisisishiwa sana kufahamu uhakika wenyewe. Madhehebu yote ya Wayahudi yanaafikiana kwamba tangu Hadhrat Musa[as] alipopewa Torati, kisha katika nyakati mbalimbali Manabii wakaendelea kufika, yeyote hakutoa fundisho la Utatu, bali wote waliendelea kufundisha kwamba Mungu wenu ni Mmoja ambaye haonekani. Wayahudi wano udhuru huu pia kwamba huko mlimani Sinai, Musa[as] alipomwomba Mwenyezi Mungu ‘Onyesha uso Wako’, hapo kwa nini Mungu Akasema kwamba hakuna yeyote awezaye kuona uso Wangu; ilimpasa Mungu kuonyesha sura ya Yesu Akisema uso wangu ndio huu. Ilmuradi, Wayahudi wametaka kuthibitisha kwamba dini ya Kikristo ni dini inayotaka kuchana Agano la Kale la

Torati walilotilia mihuri Manabii wote, na jiwe la msingi la Torati lililo tauhidi wanatamani kuling'olea mbali. Kwa kifupi, Wakristo wakileta mungu wa aina hii ambaye mafundisho yake kuhusiana na Mungu hayalingani kamwe na mafundisho ya Torati wala Kurani, wametaka kueneza duniani bidaa makuruhu. Hawajali hata kidogo kwamba ikiwa itikadi mpya kama hiyo imepingwa na Torati na vitabu vya Manabii wengine, basi kwa uchache ingethibitishwa kwa akili, bali kuhusu akili pia uzembe wao ni wa ajabu, kana kwamba kwao hoja ya kiakili haina madaraka juu ya dini; bali kwao akili haistahiki kuweza kutoa ushahidi wowote kuhusu tauhidi na Utatu. Hao wamezoea sana kukosoa wengine, lakini ni ajabu kwamba kuhusu itikadi yao hawatafakari hata kidogo. Iliwapasa kuthibitisha kwanza uungu wa Bwana Yesu, unaokadhibishwa na Torati, Kurani na akili, zote tatu, kisha wangesisitiza mambo yaliyobuniwa – kafara, wokovu na kadhalika. Lakini, hawakufanya hivyo, na kwa kutokujali msingi hasa wa itikadi yao wakashughulikia mambo ya upuuzi. Lakini pamoja na hayo ningependa kueleza pia kwamba chini ya kosa hili upo ukweli pia uliofichika. Na ingawaje ukweli huo umeaibishwa sana hata kwamba sasa badala ya uzuri, sura yake mbaya na ya kutisha inaonekana, hata hivyo ndani ya mawingu meusi mna nuru ya umeme ya ukweli kwa hakika inayoonekana kidogo kuyafanya mafundisho yake ya kuhilikisha

yamfanye Yesu kuwa mungu. Nayo ndiyo kwamba inathibitika kutoka katika Torati kuwa Mungu Alimwumba mwanadamu kwa sura yake na akamtilia nuru yake na kumpulizia roho yake. Na Kurani Tukufu pia yaeleza hivyo. Siyo zaidi ya uwezo na asili ya kibinadamu kwamba Mungu Ateremke kijalali katika moyo safi wa mja wake kwa njia hii kwamba hema la adhama Yake likite moyoni mwake, na kati ya Mungu na mja wake uhusiano wa namna hii uzalike kama vile, kwa mfano, chuma kinapotiwa katika moto mkali uwakao, hapo kidhahiri kinaonekana kama moto, lakini hata hivyo kwa hakika hicho ni chuma tu si moto. Basi, kwa hakika uhusiano huu huu wapenzi kamili wa Mungu wanakuwa nao na Mungu, na huanza kuhisi ndani mwao kwamba Mungu Amewashukia ndani yao. Na baadhi ya wakati katika hali hii ya mwungano na Mungu, baadhi ya waja wamepata kutamka maneno yaonekanayo ya kufuru. Yaani, waja hao wanaeleza uhusiano ule kwa Mungu namna ambayo watu wa kawaida kwa kudangayika wanafikiri kana kwamba waja hao wanadai kuwa Mungu. Maneno ya aina hii yanapatikana takriban katika Vitabu vyote vya Mungu.

## Kauli na Amali za Mtume Mtukufu[saw]

Katika Kurani Tukufu, kwa msingi huu huu, kauli na amali za Nabii wetu[saw] zimesemwa kuwa ni kauli na amali

za Mungu. Mathalan, kuna aya hii kuhusu kauli وَ مَا يَنۡطِقُ عَنِ الۡهَوٰى اِنۡ هُوَ اِلَّا وَحۡىٌ يُّوۡحٰى[20], yaani kauli ya Nabii huyu haitoki kutoka katika chemchemi ya tamaa ya kibinadamu, bali kauli yake ni kauli ya Mungu. Angalieni sasa, sawa na aya hii, kauli zote za Mtume Mtukufu[saw] zinathibitika kuwa kauli za Mwenyezi Mungu. Na kulinganisha nayo ipo aya nyingine ambayo yathibitika kwayo kwamba matendo yake pia ni matendo ya Mwenyezi Mungu, kama alivyosema[21] مَا رَمَيۡتَ اِذۡ رَمَيۡتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى, yaani uliyotupa hukutupa, bali Mungu Alitupa. Basi, kwa aya hii imethibitika kwamba matendo pia ya Mtume Mtukufu[saw] ni matendo ya Mungu. Hivyo, ikiwa kauli za Mtume Mtukufu[saw] zimekuwa kauli za Mungu na matendo yake pia yamekuwa matendo ya Mungu, semeni sasa natija yake ndiyo nini isipokuwa kwamba Mtume Mtukufu[saw] ndiye dhihirisho kamili la dhati ya Mwenyezi Mungu. Lakini, hata hivyo, Waislamu wenye akili hawamwiti Mtume Mtukufu[saw] kuwa Mwenyezi Mungu, wala kama Wakristo, hawamwiti Mtume Mtukufu[saw] kuwa أُقْنُوْم[22] (uknuum) wa Mungu ilhali hapa kuna ushahidi wa kimatendo pia, nao ndio huu kwamba kama Mwenyezi Mungu Alivyo na

[20] Sura An-Najm 53:4-5

[21] Sura Al-Anfaal 8:18

[22] Uknuum (أُقْنُوْم) : sawa na imani ya Ukristo, Mungu ana uknuum 3: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Mwenezi

ghera kwa Dhati yake, ndivyo hivyo Huonyesha ghera kwa ajili ya Mtume[saw]. Na wale waliomwudhi Mtume[saw] na kumwaga damu bila haki na wakamfukuza nchini, Mwenyezi Mungu hakumfisha Mtume[saw] mpaka Akawaonjesha adhabu, na waliomsaidia Akawakalisha katika viti vya enzi. Sasa tunapolinganisha hali za Mtume Mtukufu[saw] kwa hali za Yesu Masihi, twalazimika kukiri kwamba Mwenyezi Mungu kwa kitendo Hakumsaidia Yesu Masihi kwa njia yoyote bali kinyume chake akaendelea kuwasaida Wayahudi hata kwamba wakamtundika Yesu Masihi msalabani na kumdhalilisha vibaya sana. Khosrow Pervez aliponuia kumwua Mtume Mtukufu[saw], akauawa mwenyewe usiku huo huo. Lakini kwa sababu ya taarifa ya uongo ya Wayahudi ilipotolewa hati ya kumkamata Yesu Masihi, basi askari mmoja au wawili tu wakamkamata Yesu Masihi katika muda wa saa tatu na kumtia gerezani. Sasa kila mtu anaweza kuelewa kwamba je mtu kama huyu alikuwa na utukufu wowote wa kiungu pia hata kwamba juu ya maombi ya usiku kucha hakuweza kusalimika kukamatwa! Kisha tunapoona kwamba kwa kumwua Nabii wetu Mtukufu[saw] watu waliojumuika nyumbani kwake kwa nia ya kumshambulia na kuzunguka nyumba yake wakashindwa juu ya juhudi zao za hali ya juu kabisa na akahifadhiwa kwa hisani ya Mungu bila kufanya maombi usiku kucha kama Yesu Masihi, na akatoka baina ya wazee hao wa

baraza wakati wa uchao na mtu yeyote hakuweza kumwona. Lakini dua yenye uchungu ya Bwana Yesu Maishi, *Eloi Eloi, lama sabakthani*, ambayo Wayahudi mpaka sasa wanaicheka, ikakataliwa hivi kwamba sawa na ikirari ya Wakristo, matokeo ya dua hii yalikuwa kwamba akasulubiwa. Hayo ndiyo Mwenyezi Mungu Aliyomtendea Bwana Yesu; na hali za wanafunzi wake pia ni za namna hiyo hiyo tu. Hao waliahidiwa kwamba bado mtakuwa hai nami nitarudi. Angalieni sasa, bishara hii ilibatilika kwa uwazi, kwani miaka elfu mbili inakaribia kumalizika, hakuna hata alama ya ujio wake. Hao wote waliomsubiri walikufa ilhali Wayahudi walidumu kuendelea kuwacheka kwamba mwalimu wenu amerudi wapi; nao daima waliaibika kuulizwa swali hili wala hawakuweza kujibu lolote. Waliahidiwa viti kumi na viwili vya enzi, lakini katika uhai wa Bwana Yesu mwenyewe mwanafunzi mmoja akaritadi na mwingine pia akatenda kama walioritadi na hivyo viti vya enzi vikabaki kumi tu ilihali katika bishara viliahidiwa viti kumi na viwili. Na Mtume wetu[saw] aliwaahidi Masahaba zake kujikalia vitini vya enzi katika dunia hii, basi hata wapinzani wetu wanajua kwamba ahadi hiyo ikapata kutimia. Ilmuradi, maneno yaliyomo ndani ya mafundisho ya Bwana Yesu ambayo kwa sababu ya hayo yeye anafanywa mungu, siyo maneno ya nadra au ya ajabu, kwani maneno ya namna hii yanapatikana sana kuhusu Manabii wengine pia. Adamu

pia ameitwa mwana wa Mungu na Israeli naye akaitwa mwana wa Mungu, bali imeandikwa katika sehemu fulani kwamba nyinyi nyote ni miungu. Lakini, je kwa maneno hayo yapasa kuchukua maana hii kwamba watu ambao maneno kama haya yametumiwa kwa ajili yao, ni miungu kwa kweli au wana wa Mungu? Bwana Yesu naye pia ametumia maneno ya namna hii tu.

**Ujio wa Masihi Mau'udi**

Ilmuradi, twalazimika kusema kwa masikitiko makubwa kwamba kuhusu Bwana Yesu imepigwa chuku pasipo haki. Angalieni, mimi pia napata ufunuo kutoka kwa Mungu na tangu zaidi ya miaka ishirini Mwenyezi Mungu Anaongea nami; ishara karibu mia na hamsini zimedhihiri. Nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wafu kama wale walioendelea kuhuika sawa na suna ya Mungu, wakahuika kwa njia yangu pia. Kadhalika, naweza kusema kwa kuapa kwamba maombi yangu zaidi ya elfu kumi yamekubalika. Na maneno yaliyotumika katika Injili kuhusu Yesu Masihi ambayo kwayo uungu wake unathibitishwa, kuzidi sana hayo Mwenyezi Mungu Ametumia maneno kuhusu mimi, nami nimetangaza pia maneno kama hayo kupitia vitabu. Mungu Ameniita Adamu; Mungu Ameniita Ibrahimu; Mungu Ameniita Masihi Mau'udi; na akatoa habari kwamba wewe ndiwe yule aliyeahidiwa ambaye kwa

kumongejea Manabii wote wamepita. Lakini hata hivyo, sisemi kwamba ni Mungu mie au mwana wa Mungu, ilhali kunihusu mimi yapo maneno mengi ndani ya maneno ya Mungu, ambayo kwayo naweza kuitwa Mugu kuliko Masihi mwana wa Mariamu, lakini najua hii ni kufuru. Kwa hiyo, nashangaa zaidi kuliko dunia nzima kwamba Msihi mwana wa Mariamu alikuwa na fadhila gani maalumu ambayo kwayo alifanywa Mungu. Je alikuwa na miujiza mahususi? Lakini, naona miujiza iliyozidi kuliko yake yaendelea kudhihri hapa. Je, bishara zake zilikuwa bora za hali ya juu? Lakini nitasema kinyume cha uhakika nisipokubali kwamba bishara nilizojaliwa zinazidi sana kuliko za Masihi mwana wa Mariamu. Je naweza kusema kwamba katika Injili yamo maneno yaelezayo juu ya shani ya adhama kubwa ya hali ya juu ya Masihi mwana wa Mariamu yanayolazimisha kumkubali yeye kuwa Mungu? Lakini nasema kwa kuapa kwa Mungu ambaye kuapa kiapo chake cha uongo kunasababisha laana katika dunia na ahera, kwamba maneno yaliyonenwa na Mwenyezi Mungu kuhusu adhama yangu – ambayo kuhusu hayo nasema tena kwa kuapa kwamba ndiyo maneno halisi ya Mungu, yasiyogeuzwa na kubadilishwa kama Injili – yanazidi sana kueleza adhama kuliko yale wanayoyaonyesha mapadri katika Injili kuhusu Masihi mwana wa mariamu. Lakini je,

yanijuzu mimi nidai kuwa Mungu au niitwe mwana wa Mungu? Hivyo, mwelewe kwa yakini kwamba Masihi mwana wa Mariamu pia si mwana wa Mungu wala Mungu. Mimi ni **Masihi wa Muhammad** na yu **Masihi wa Musa**. Takdiri ya Mungu ilipanga hivi kwamba mwishoni mwa silsila ya Kiisraeli ambayo sheria yake ilianzia na Musa, aje Masihi, na kulingana na hii ilipangwa pia kwamba mwishoni mwa silsila ya Kiismaili pia ambayo sheria yake ilianzia na Muhammad Mteule[saw], aje Masihi. Basi ikawa hivyo hivyo. Musa, mja wa Mugu, akaleta sheria kwa wana wa Israeli. Mungu Alijua kwamba karibu ya karne ya kumi na nne kutoka Musa, wana wa Israeli watatupilia mbali kweli za sheria na siri zake, na hali yao ya kihulka itakuwa mbaya sana. Basi, kwa lengo hili Mungu akamwumba Masihi mwana wa Mariamu katika karne ya kumi na nne kuanzia Hadhrat Musa ndani ya nchi ambamo utawala wa Wana wa Israeli pia haukubaki. Basi, sawa na ahadi ya kumbukumbu la Torati, mfano wa Musa alipofika duniani, yaani Hadhrat Muhammad Mteule[saw], ndipo baada yake pia ilipowadia karne ya kumi na nne, Mungu akamwumba Masihi, mfano wa Masihi wa kwanza, na huyo ndiye **mimi.** Na kama vile mfano wa Musa alivyomzidi Musa katika mambo mengi, ndivyo hivyo mfano wa Isa pia katika

mambo mengi akamzidi Isa, na fadhila hii katika baadhi ya mambo Mungu Anampa Amtakaye.

**Umaasumu Wawezaje Kuthibitika**

Sasa naona kwamba masiala ya umaasumu na uombezi yanayoletwa na Wakristo mara kwa mara, ni udanganyifu kabisa walioangukia hao Wakristo. Kama maasumu maana yake ni kwamba adui yeyote asikosoe maisha yake, basi njooni tukawaonyeshe vitabu vya Wayahudi waliokosoa sana mienendo ya Bwana Yesu na mama yake. Na kama maana ya maasumu ni hii kwamba mtu aseme kwa kinywa chake kwamba mimi ni mwema, basi njooni tukawaonyesha katika Injili kwamba Bwana Yesu alikiri kuwa yeye si mwema. Basi, umaasumu wa Masihi mwana wa Mariamu usipoweza kuthibitika kwa njia yoyote, bali sawa na Injili baadhi ya matendo yake yathibitika kinyume cha umaasumu wake, kama vile kunywa pombe, kuvunja amri ya kudumu ya uharamu wa nguruwe na amri ya tohara na kadhalika, kuharibu mali ya wengine, kuwatukana waandishi na mafarisayo, kuwapa fursa wanawake malaya kugusa mwili wake, kuruhusu kupakwa mafuta ya haramu kichwani, kutowakataza wanafunzi kuvunja masuke katika mashamba ya watu. Sasa semeni, mambo hayo yote ni dhambi au la. Ikiwa kunywa pombe ilikuwa kazi nzuri, mbona Yohana akaichukia. Danieli akasema, wanywa pombe hufungiwa

milango ya mbinguni. Tohara iliyokuwa amri ya kudumu, kwa nini akaikataza ilihali sawa na utafiti wa kisasa pia hii inafaa dhidi ya maradhi mengi. Kadhalika, nguruwe alikuwa haramu kwa kudumu, kwa nini akatoa fatuwa ya kula nyama yake, ilhali mwenyewe alisema kwamba Torati haikutanguliwa, tena mwenyewe akaitangua. Na yapasa kukumbuka kwamba kuthibitisha umaasumu wa Bwana Yesu mwana wa Mariamu sawa na Injili ni mushkili kama vile kuthibitisha afya ya mwenye kifua kikuu ambaye kwa maradhi yake ametoka mabebe na ana tumbo la kuendesha. Je, haikuwalazimu kuthibitisha kwanza umaasumu wa Bwana Yesu, kisha baadaye wangewakosoa wengine. Kwa kuona tu neno la *istighfar* katika Kurani, haraka sana kudai kwamba hili lathibitisha kufanya dhambi na kujifanya hawakuiona kauli hii ya Yesu katika Injili kwamba mimi si mwema. Je huu ni uaminifu? Kisha, baada ya hayo yote twaona pia kwamba mwombezi wa akhera anaweza kuthibitika yule aliyewahi kuonyesha mfano wowote wa uombezi duniani. Basi, kwa kuzingatia kigezo hiki tunapomwona Musa, yeye naye pia huthibitika mwombezi, kwani mara kwa mra akaondoa adhabu ishukayo. Torati ni shahidi juu yake. Kadhalika tunapomwona Hadhrat Muhammad Mteule[saw], basi kuwa kwake mwombezi kwaonekana kuwa ni dhahiri shahiri yenyewe, kwani hii ilikuwa ni athari ya uombezi wake kwamba akawakalisha Masahaba zake

waliokuwa maskini katika kiti cha enzi; na ilikuwa ni athari ya uombezi wake kwamba ingawaje watu hao walilelewa katika ibada ya masanamu na shirki, wakawa waaminio wa tauhidi ambao mfano wao haupatikani katika zama zozote. Tena ilikuwa ni athari ya uombezi wake kwamba mpaka sasa wafuasi wake hupokea ufunuo wa kweli wa Mungu, Mungu Huongea nao. Lakini katika Yesu mwana wa Mariamu tunawezaje kupata ithibati hii yote na kwa njia gani? Juu ya uombezi wa Seyidi na kiongozi wetu Muhammad Mteule[saw] utakuwa ushahidi upi zaidi na imara kuliko huu kwamba tuyapatayo kutoka kwa Mungu kumpitia yeye, hawawezi kuyapata wapinzani wetu. Kama wapinzani wetu wakiujia mtihani huu, basi katika siku chache uamuzi unawezi kufanyika; lakini hawataki uamuzi. Hao wanatulazimisha kumwamini mungu yule asiyeweza kusema wala kuona wala kutoa habari yoyote mapema. Lakini Mungu wetu Yu Mweza wa mambo hayo yote. Abarikiwe yule amtakaye Mungu wa aina hii.

(Kutoka Review of Religions, jalada 1, namba 5, Mei 1902, uk. 175 hadi 209)